

## **FASIHI KWA UJUMLA**

**Dhana ya fasihi:** Fasihi ni sanaa au ni tawi la sanaa linalotumia lugha katika kufikisha ujumbe wa msanii kwa hadhira.

- **Msanii ni nani?** Msanii (fanani) ni mtu yeyote anayetunga kazi za kisanaa.
- **Hadhira ni nani?** Hadhira ni wapokeaji wa kazi za kisanaa. Hadhira, wanaweza kuwa ni wasomaji au wasikilizaji/Watazamaji.

### **SANAA**

Sanaa ni uzuri unaojitokeza katika umbo lililosanifiwa na msanii. Mfano, uchoraji, uchongaji, ususi na kadhalika.

### **AU**


Ni ufundu wa kuwasilisha mawazo yaliyo katika fikra za binadamu.

### **AINA ZA SANAA**

Kuna aina tatu (3) za sanaa;

- (i) **Sanaa za ghibu;** ni aina ya sanaa ambayo uzuri wake hujitokeza kwa kusikiliza. Mfano, muziki, mashairi.
- (ii) **Sanaa za maonesho;** ni aina ya sanaa ambayo uzuri wake hujitokeza kwa kuona. Mfano, uchoraji, ususi, ufinyanzi.
- (iii) **Sanaa za vitendo;** ni sanaa ambayo uzuri wake hujitokeza kwa kuona na kusikiliza. Mfano, maigizo, tamthiliya.

### **MCHORO WA SANAA**



Kutokana na maelezo hayo hapo juu, inadhihirisha kabisa kuwa fasihi ni tawi la sanaa na hasa ukiangalia katika mchoro wa sanaa, utakuta kuna kipengele cha fasihi ndani yake.

### **Swali: Kwanini fasihi ni sanaa?**

Usanaa wa fasihi, unajidhiihiha katika mambo yafuatayo;

- ***Uteuzi mzuri wa lugha;***

kwa kawaida kazi za fasihi, iwe fasihi simulizi au fasihi andishi huwa na lugha yenye ufundi, lugha hii huwavutia hadhira katika kuisikiliza au kuisoma kwake. Lugha ya kifasihi ni lugha iliyojaa matumizi ya methali, misemo, nahau na tamathali mbalimbali za semi na kadhalika.

- ***Mpangilio wa wahusika;***

Wasanii wa kazi za kisanaa hutumia ufundi wa kuwapanga wahusika ili wasaidie kufikisha ujumbe kwa hadhira zao. Wasanii huweza kuwachora wahusika halisi au wahusika wa kubuni na kuwapa majukumu yenye ufundi mkubwa kwa hadhira.

- ***Msuko wa visa na matukio;***

Maranyingi wasanii wa kazi za kifasihi hupanga matukio yao katika kazi zao kwa kutumia ufundi mkubwa. Wasanii wanaweza kupanga kazi zao moja kwa moja au kurukiana. Kitendo hiki hufanya baadhi ya wasomaji kuweza kuburudika zaidi pindi wanaposoma kazi hizo.

- ***Ubunifu;***

Mawazo aliyonayo msanii wa kazi za kifasihi yanatumia ubunifu mkubwa katika kuyawasilisha kwa hadhira. Mawazo hayo yanaweza kuibua furaha au huzuni kwa msomaji au msikilizaji.

- ***Uteuzi mzuri wa mandhari;***

Hata katika kuiteua mandhari katika kazi ya fasihi huhitaji ufundi. Wasanii huweza kutumia mandhari halisi au ya kubuni. Maranyingi, wasanii huchora mandhari, hata yakiwa ya kubuni lakini husadifu mandhari ya kawaida. Kitendo hicho hudhihirisha usanaa wa fasihi.

### **Swali: Eleza tofauti kati ya fasihi na sanaa nyingine**

Ukiangalia katika mchoro wa sanaa, utaona kuna kipengele cha fasihi na sanaa nyinginezo kama vile; ususi, uchongaji, utarizi na kadhalika. Sasa swali la kujiuliza ni kwamba, sanaa hii ya fasihi inawezaje kutofautiana na sanaa nyinginezo?

#### **Lugha;**

Ni kitu pekee kiachoweza kutofautisha kati ya fasihi na sanaa kama vile, uchongaji, ususi, ufinyazi na kadhalika. Ili iwe kazi ya fasihi ni lazima itumie lugha, iwe lugha ya mazungumzo au maandishi. Lakini sanaa kama uchongaji haitumii lugha katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira husika.

- ***Utendaji;***

Kazi ya fasihi, huwa na utendaji yaani vitendo halisi hupatikana. Mfano, maigizo, miviga na kadhalika. Utendaji huu wa kazi za fasihi hushirikisha fanani na hadhira kwa wakati mmoja hasa katika fasihi simulizi. Tofauti na sanaa nyingine ambazo huwezi kuupata utendaji na ushirikishwaji wa fanani na hadhira kwa wakati mmoja.

**-Fani na maudhui;**

Kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na maumbo mawili ambayo ni fani na maudhui. Hakuna kazi ya fasihi ambayo haina fani na maudhui. Tofauti na sanaa nyingine ambazo si lazima kuwa na vipengele hivyo vya fani na maudhui.

**-Wahusika;**

Katika kazi ya fasihi wahusika wanaweza kuwa ni viumbe hai au visivyokuwa na uhai hasa katika fasihi simulizi. Sanaa nyingine haina uwezo wa kutumia viumbe hai na wasiokuwa na uhai.

**- Mandhari;**

Katika fasihi mandhari yanaweza kuwa halisi au ya kubuni. Katika sanaa nyingine inaweza kuwa na mandhari ya aina moja tu au kukosa kabisa mandhari.

- Kutoka na maelezo hayo, tunaweza kuhitimsha kwa kusema, “Fasihi ni tawi la sanaa linalotumia nyenzo ya lugha katika kufikisha ujumbe wa msanii kwa hadhira husika”.

### **AINA ZA FASIHI**

Kwa kawaida fasihi ni moja, lakini kutokana na uwasilishaji wake tunaweza kupata aina mbili(2) za fasihi;

- (a) Fasihi simulizi.
- (b) Fasihi andishi.

(a) **Fasihi simulizi**

Ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo au masimulizi katika kufikisha ujumbe wa msanii kwa hadhira. Mfano, hadithi, ushairi, maigizo na sanaa mbalimbali za monesho.

***Sifa za fasihi simulizi***

Fasihi simulizi ina sifa za pekee zinazoweza kutofautisha na aina nyingine ya fasihi. Sifa hizo ndizo huipa uhai fasihi hii. Miogoni mwa sifa hizo ni pamoja na:

- = **Utendaji;** Fasihi simulizi huwa na utendaji, yaani vitendo halisi hupatikana. Utendaji wa fasihi simulizi hushirikisha fanani na hadhira kwa wakati mmoja.
- = **Uwepo wa fanani na hadhira;** Fasihi simulizi hukutanisha fanani na hadhira kwa wakati mmoja- Fanani huweza kusimulia, kupiga makofi na hata kubadilisha miondoko na mitindo ya usimuliasi. Hadhira huweza kushiriki kwa kuuliza maswali, kupiga makofi, kushangilia kuimba na kadhalika kutegemeana na jinsi ambavyo fanani atawashirikisha.

**Swali:** -Fafanua sifa za hadhira wa fasihi simulizi.

-Hadhira wa fasihi simulizi wanatofautiana vipi na hadhira wa fasihi andishi?

- = **Hubadilika kutokana na wakati na mazingira;** Baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hubadilika kulingana na wakati. Mfano, msimuliasi wa hadithi anaweza kusimulia

hadithi kulingana na wakati uliopo. Au nyimbo nyingi hutungwa kulingana na maudhui yanayojitokeza katika wakati huo. Nyimbo za wakati wa ujamaa ni tofauti kabisa na nyimbo za wakati wa utandawazi. Kwa upande wa mazingira, nayo husababisha kubadilika kwa fasihi simulizi. Mtu anaweza kutoa msemo kwa kuhusisha mazingira ya vitu vilivyomzunguka. Mfano msemo usemao, "Pilipili usoziла за kuwashia nini?" Msemo wa namna hii umekuja kutokana na mazingira hayo ya pilipili.

**Swali: "Fasihi simulizi hubadika kutokana na mazingira na wakati". Jadili**

= **Huzaliwa, hukua na hata kufa;** kuzaliwa kwa fasihi simulizi hutokana na mambo yanayotokea katika jamii. Kukua: Fasihi simulizi hukua kadiri inavyoyajadili matatizo yaliyomo katika jamii. Kufa: Fasihi simulizi hufa kwa namna mbili. Hii ni kutokana na maendeleo ya mazingira ambayo hufuata mfumo wa jamii husika. Mfano, maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pili ni kupoteza mbinu zake za kisanaa.

**Swali: Eleza ni kwa jinsi gani maendeleo ya sayansi na teknolojia yanavyoweza kuathiri fasihi simulizi.**

= **Ni mali ya jamii nzima;** Fasihi simulizi humilikiwa na kila mtu katika jamii. Sifa hii ndiyo huipa uwezo kurithishwa toka kizazi kimoja kwenda kingine.

= **Ina uwanja maalumu wa kutendea;** Fasihi simulizi huwa na sehemu rasmi ambayo imetengwa kwa ajili ya kipera Fulani cha fasihi simulizi. Sehemu hiyo inaweza kuwa porini, msituni, mtoni, pangoni, nyumbani na kadhalika.

= **Ina utegemezi;** utegemezi wa fasihi simulizi hutegemea zaidi sanaa za maonesho hasa sanaa za ghibu yaani muziki, kwa sababu fasihi simulizi huchota uhai wake kutokana na vitendo na tabia za fanani, mahadhi na toni za kimuziki na vipengele vingine vya sanaa za maonesho.

### **Dhima za fasihi simulizi**

Fasihi simulizi huwa na umuhimu mkubwa katika jamii. Umuhimu wa fasihi simulizi hupatikana kupitia tanzu zake. Umuhimu huo ni kama ufuataeo:

- **Kuelimisha jamii;** Fasihi simulizi huelimisha jamii, watu wanaweza kuelimika na kufahamu mambo mbalimbali yanayojitokeza kwa jamii kupitia fasihi simulizi. Ukiangalia katika utanzu wa hadithi, jamii inajifunza mambo mbalimbali ambayo vizazi vilivyopita vilifanya na jamii inaweza kuelimika kwa kujua mambo hayo yaliyofanyika katika wakati huo.
- **Huburudisha jamii;** jamii inaweza kuburudika kupitia kazi mbalimbali za fasihi simulizi, kwa mfano, mtu akiwa anasikiliza nyimbo kupitia utanzu wa ushairi hapo huwa anaburudika. Watu wanaweza kuburudika kwenye fasihi simulizi hata kwa kuangalia miondoko ya wachezaji au matendo yoyote yanayofanyika katika utanzu huo.
- **Huadibu watu katika jamii;** kupitia tanzu za fasihi simulizi, jamii hasa watoto wanaweza kuaswa na kuwa na tabia njema. Zipo hadithi, nyimbo na kadhalika, zote hizi husaidia kutoa adabu njema kwa jamii hasa jamii ikiwa inasikiliza na kutazama kazi hizo.

- **Hutunza historia ya jamii;** jamii inaweza kutambua asili ya mwenendo wa maisha ya sasa kupitia fasihi simulizi. Bado kuna mambo ambayo yanaendelea kutendeka katika jamii zetu kwa sababu ya mila na desturi za watu wa zamani. Fasihi simulizi hutusaidia kutunza historia hiyo kupitia matambiko, miviga na kadhalika.
- **Kukuza lugha;** Fasihi simulizi hutumia lugha kufikisha ujumbe wake katika jamii, lugha ya fasihi huwa ni ya kisanaa zaidi na hivyo kuifanya iwe yenye mvuto kwa wasikilizaji au wasomaji. Mtu anaposoma au kusikiliza kazi ya fasihi anapata ujuzi wa lugha. Lakini pia fasihi yenyewe inaweza kutumika kama chombo cha kukuza lugha. Wasimulizi na waandishi wa fasihi huhitaji kuwa na utajiri mkubwa wa lugha.
- **Kukuza uwezo wa kufikiri;** vipera vingi vya fasihil simulizi huwachochea hadhira kufikiri sana ili kuweza kupata suluhisho. Mfano, methali, vitendawili na kadhalika.
- **Hutoa mchango mkubwa katika fasihi andishi;** waandishi wa kazi za fasihi andishi, hutumia vipengele vya fasihi simulizi katika kazi zao za fasihi andishi. Kwa mfano, methali, vitendawili, hadithi na kadhalika.

### **MASWALI:**

1. Fafanua dhima tano (5) za fasihi simulizi katika jamii.
2. “Moja ya dhima ya fasihi simulizi ni kuelimisha jamii”. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja tano.
3. Fafanua mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi.

### **Wahusika wa fasihi simulizi**

Fasihi simulizi huweza kujengwa kwa wahusika wafuatao:

- i) **Msimuliasi (Fanani):** Huyu ni mhusika katika fasihi simulizi, kazi yake kubwa ni kuwaslisha mawazo aliyonayo kwa hadhira. Msimuliasi hujitahidi kutumia mbinu mbalimbali kwa ajili ya kujenga kazi yake. Mfano wa mhusika huyu ni Mtambaji wa hadithi, mwimbaji na kadhalika.
- ii) **Wasikilizaji (Hadhira):** Hawa ni wale wapokeaji wa kazi ya fasihi. Maranyingi kazi yoyote ya fasihi hutungwa kwa kuwahuusu wao. Uhusika wao hujitokeza kwa namna mbili; kwanza ni kusikiliza na pili ni kushiriki katika baadhi ya matendo kama vile; kupiga makofi, kuimba, kuuliza maswali na kadhalika.
- iii) **Wanyama na viumbe wengine:** Fasihi simulizi hutumia wanyama na viumbe wengine kama njia ya kupitishia ujumbe kwa hadhira. Mfano, Sungura, Fisi, Simba na kadhalika. Maranyingi tanzu za fasihi simulizi, kwa mfano utanzu wa hadithi hutumia sana viumbe hao ili kufikishia ujumbe. Fasihi simulizi hutumia wanyama kwa sababu zifuatazo:
  - Kuepusha migogoro kwa jamii, ikiwa fasihi simulizi ingalimtaja mtu anayehusiana na tabia mbovu iliyojadiliwa, jamii ingalikuwa katika migogoro.
  - Hulka au tabia za binadamu znafanana na wanyama, wanafasihi wengi wa fasihi simulizi hutumia wanyama kwa kuwa binadamu na wanyama wanafanana katika baadhi ya tabia. Mfano, uroho – Fisi. Ujanja –Sungura.

- Binadamu alikuwa karibu sana wanyama, tangu mwanzo binadamu alikuwa karibu sana na wanyama, hivyo ilikuwa rahisi kwa mwanafasihi wa fasihi simulizi kutunga kazi yake na kumtolea mfano mnyama.
- iv) **Vitu na mahali:** Fasihi simulizi hutumia vitu na mahali katika kufikishia ujumbe wake. Mfano, katika hadithi nyingi za fasihi simulizi vitu visivyo na uhai hupewa uhai. Unaweza kusikia katika hadithi jive linaongea na kadhalika.
- v) **Binadamu:** Hawa ni wahusika wa fasihi simulizi, wahusika hujadiliwa ndani ya tukio la kifasihi, mfano: Katika hadithi anaweza akatajwa mtu, mtu huyoanaweza kuwa ni mfalme au mtoto wa mfalme. Kwa kawaida binadamu anayezungumziwa katika tukio hilo la fasihi simulizi ndiye anayebeba maudhui ya kazi nzima.


### **MASWALI:**

1. Fafanua wahusika watano (5) wa fasihi simulizi
2. Fasihi simulizi hutumia wanyama katika uwasilishaji wake lakini maudhui yake yanamhusu binadamu. Jadili
3. Elezea kwanini wanafasihi wa fasihi simulizi hutumia wahusika wasiokuwa binadamu kufikisha ujumbe kwa hadhira zao? Toa hoja nne.

### **Tanzu za fasihi simulizi**

Fasihi simulizi imegawanyika katika tanzu (matawi) manne (4) ambayo ni:

- (a) Hadithi
- (b) Semi
- (c) Ushairi
- (d) Sanaa za maonesho /Maigizo



### **(A) HADITHI**

Ni tungo za fasihi simulizi zitumiazo lugha ya nathari (lugha ya ujazo ya maongezi ya kila siku). Masimulizi hayo hupangwa katika mtiririko unaokamilisha kisa. Hadithi huwa na wahusika ambaeo ni nyenzo kuu ya kukiendesha kisa chenyewe. Wahusika wanaweza kuwa wanyama, binadamu na kadhalika.

### Sifa za hadithi

- **Huwa na mianzo na miishio maalumu:** Hadithi nyingi katika fasihi simulizi huwa na mianzo na miishio maalumu. Lengo la mianzo ya hadithi ni kuwaandaa wasikilizaji wa hadithi ili kuwa pamoja katika usimulizi.
- **Husimuliwa kwa lugha ya nathari na kwa njia ya mdomo:** Hadithi za fasihi simulizi hutumia lugha ya kawaida na ni lugha ya maongezi ya kila siku. Na mara zote hutumia mdomo katika uwasilishaji wake.
- **Huwa na wahusika ambao wanaweza kuwa ni viumbe hai au wasiokuwa na uhai:** Kama tulivyoona katika wahusika wa fasihi simulizi, hadithi huweza kutumia wahusika binadamu au wasiokuwa binadamu kwa lengo la kufikisha maadili kwa binadamu. Hapa, ikumbukwe kwamba wahusika wote wasiokuwa binadamu hupewa uwezo wa kibinadamu.
- **Huwa na funzo fulani:** Hakuna hadithi isiyokuwa na mafunzo kwa jamii. Hivyo, hadithi huwa na funzo lililokusudiwa na msimuliasi wa hadithi hiyo.
- **Hujumuisha tanzu nyininge za fasihi simulizi:** Hadithi huchota tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Msimulizi wa hadithi anaweza kutumia nyimbo, methali, misemo kwa ajili ya kuipamba kazi yake.

### MTAMBAJI WA HADITHI

Mtambaji wa hadithi: Ni mtu yejote anayefanya kazi ya kusimulia hadithi. Mtambaji wa hadithi anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- **Lazima awe mahiri wa lugha:** Mtambaji wa hadithi anatakiwa kuijua lugha anyoitambia hadithi vizuri ili aweze kutamba hadithi hiyo bila kusita.
- **Lazima ashirikishe hadhira:** Mtambaji wa hadithi anapaswa kuwashirikisha hadhira kwa kuwauliza maswali, kuwaimbisha na kadhalika.
- **Lazima awe mcheshi:** Msimulizi wa hadithi ni lazima awe mcheshi na jamii ili hadhira iweze kusikiliza hadithi bila ya kuchoka.
- **Lazima awe na uwezo wa kuigiza matendo:** Mtambaji wa hadithi anatakiwa awe na uwezo wa kuigiza baadhi ya mambo kwa kutumia ishara kutofautisha sauti, matumizi ya maleba, kubadilisha matendo na miondoko.
- **Lazima awe na uwezo kudadisi mapokeo ya hadithi yake:** Hapa mtambaji wa hadithi anatakiwa awe na uwezo wa kuidadisi hadhira yake ili aijue hadhira yake jinsi inavyoipokea hiyo hadithi. Kitendo hicho kitamfanya mtambaji wa hadithi abadilishe au aongeze pale panapohitajiwa kitu.

### USIMULIZI

Usimulizi: Ni kuelezea mtu au watu jambo ambalo limetokea hivi karibuni au zamani. Kutokana na fasili hii tunapata aina mbili za usimulizi:

- (i) Usimulizi wa hadithi
- (ii) Usimulizi wa habari

## **I. USIMULIZI WA HADITHI**

Usimulizi wa hadithi; ni kitendo cha kusimuliana hadithi, yaani visa na matukio.

### **Mbinu za usimulizi wa hadithi**

Usimulizi wa hadithi hufanyika kwa kutumia mbinu tofauti za kisanaa. Mbinu hizo hufanya usimulizi uwe na mvuto kwa hadhira. Mbinu hizo ni pamoja na:

- Kujua muundo wa hadithi:**

Kimuundo, hadithi huwa na sehemu tatu(3) ambazo ni:

- **Mwanzo wa hadithi;** huwa na maneno ya utangulizi, lengo la maneno hayo ya utangulizi ni kuianda hadhira ili kuvuta umakini na usikivu wa hadithi hiyo.

- Mfano:**

Hadithi...Hadithi!

Paukwa.....

- **Kiini cha hadithi;**baada ya kumaliza maneno ya utangulizi fanani huanza kusimulia hadithi yake. Maranyingi, fanani huanza kwa maneno yafuatayo:  
FANANI: “Hapo zamani za kale”  
HADHIRA: Enheee!
  - **Mwisho wa hadithi;** baada ya kumalizika kwa hadithi fanani humaliza kwa mwisho maalumu. Maranyingi usimulizi wa hadithi huishia kwa maneno yafuatayo:  
“ Hadithi yangu imeishia hapo”

- Kujua mbinu za kisanaa za usimulizi:**

Mbinu za kisanaa za usimuliasi wa hadithi ni pamoja na:

- Uigizi:**

Katika usimulizi wa hadithi, uigizi unahusisha uigaji wa sauti za viumbe wanaosimuliwa katika hadithi, miondoko yao, matendo yao, mavazi yao na kadhalika. Msimulizi wa hadithi hutakiwa kuzingatia hayo wakati wa usimulizi wake.

- Michepuko:**

Mchepuko katika usimulizi wa hadithi ni namna ya kuacha kwanza kusimulia hadithi moja kwa moja na kuongelea mambo mengine kwa ufupi. Kutolea mifano ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha halisi ya jamii.

- Lugha ya kisanaa:**

Usimulizi wa hadithi hutakiwa kutumia lugha ya kisaa ili kumvuta msikilizaji, hivyo fanani anayetamba hadithi ni yule anayeijua lugha vizuri ya kisanaa ili kumvuta hadhira.

- Kushirikisha hadhira:**

Usimulizi wa hadithi sharti ushirikishe hadhira, njia za kuishirikisha ni:

- Kuiuliza maswali hadhira
- Kuiimbisha hadhira

- **Uzingatiaji wa sauti:**

Utambaji wa hadithi sharti uzingatie sauti inayosikika. Mtambaji wa hadithi katika usimulizi wake hukaa mbele ya hadhira, na kutoa sauti inayosikika.

Matumizi ya sauti yanajumuisha:

- Utoaji wa sauti inayosikika
- Matumizi ya viimbo

### **FANI KATIKA HADITHI**

Hadithi za fasihi hujengwa kwa fani na maudhui. Fani katika hadithi hujengwa kwa vipengele vifuatavyo:

(a) **Muundo wa hadithi;**

Muundo wa hadithi za fasihi simulizi ni wa moja kwa moja, ambao una mwanzo, kati na mwisho.

- Mwanzo

Mwanzo wa hadithi huanza na maneno maalumu. Mfano:

Mtambaji: Hadithi... Hadithi....!

Hadhira: Hadithi njoo! Utamu Kolea

#### Au

Mtambaji: Paukwa.....!

Hadhira: Pakawa.....!

- Kati

Hapa habari zote kuhusu hadithi huelezwa hapa. Hapa matukio muhimu husimuliwa kwa kufuata maelezo ya moja kwa moja.

- Mwisho

Hapa msimuliaji wa hadithi huonesha mafanikio au matatizo yaliyomkuta mhusika.

Msimulizi humalizia kwa kusema, “Hadithi yangu imeishia hapo”.

(b) **Mtindo wa hadithi:**

Hadithi za fasihi simulizi hutumia mbinu mbalimbali za masimulizi. Mbinu hizi ni kama vile, matumizi ya nyimbo, matumizi ya dayolojia na kadhalika.

(c) **Wahusika:**

Wahusika wa hadithi za fasihi simulizi ni wanyama, mimea, miti, mawe, wadudu, binadamu na kadhalika. Wahusika hawa huweza kugawanya katika mafungu mawili. Yaani, wahusika wema na wahusika wabaya.

(d) **Matumizi ya lugha:**

Katika hadithi, matumizi ya lugha yapo ya aina mbalimbali. Kuna matumizi ya misemo, nahau, methali, tamathali mbalimbali za semi na mbinu nyingine za kisanaa.

(e) **Mandhari:**

Kwa ujumla katika fasihi simulizi, mandhari hayapewi nafasi kubwa, ingawa huweza kutaja mahali kama vile; porini, pangoni na kadhalika. Maranyingi mandhari ya fasihi simulizi hupambanishwa na muktadha wa wakati.


## **UMUHIMU WA HADITHI**

- Kujenga jamii na kuipa mwelekeo.
- Huelimisha, huadibu na kuonya jamii.
- Husisitiza ushirikiano katika jamii.
- Ni chombo kimojawapo cha kurithisha amali za jamii (mila na desturi)
- Hutumika kama chombo cha kuliwaza na kuondoa majonzi.

## **VIPERA VYA HADITHI**

Hadithi hujengwa kwa vipera vifuatavyo:

- (a) Ngano
- (b) Vigano
- (c) Visasili
- (d) Tarihi
- (e) Soga



### **➤ NGANO**

Ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu katika kuelezea au kuonya kuhusu maisha. Hizi ni hadithi za maadili ambazo husimuliwa katika mazingira ya starehe, nazo huadili watu katika maisha.

Maranyingi hadithi za ngano mwisho wake huwa ni wa kufurahisha.

### **Sifa za hadithi za ngano**

- Hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Huwa na watusika wanyama, wadudu, ndege, mazimwi, binadamu na kadhalika.
- Huwa na mianzo maalumu.
- Mwisho wake maranyingi huwa ni wa kufurahisha.
- Huweza kutumia mbinu mbalimbali, kama vile nyimbo, dayolojia na kadhalika.

### **Kanuni za utunzi wa hadithi za ngano**

Ngano hutungwa kwa kuzingatia kanuni zifuatazo:

- ❖ **Dhamira:** Mtunzi wa ngano anapaswa kuweka dhamira ambazo ni wazo kuu au funzo kuu. Wazo kuu huweza kujitokeza kama onyo, ushauri, himizo, tahadhari na kadhalika.
- ❖ **Wazo:** Mtunzi ni lazima abuni fikra au mawazo akilini na kuwasilisha funzo kuu kwa namna ya kufurahisha au kuhuzunisha.
- ❖ **Maudhui:** Mtunzi anapaswa kutafuta maudhui au ujumbe wa kuitisha au unaobebwa na hadithi. Kwa kawaada huwa ni maadili yaani mafundisho juu ya mwenendo mwema katika jamii.
- ❖ **Fani:** Katika fani, hapa hujumuisha mbinu za kusukia ngano. Baadhi ya mbinu hizo ni:
  - **Umbo;** ngano huhitaji kuwa na sehemu kuu nne
    - **Kichwa**  
Kichwa cha hadithi lazima kiwe ni cha kuvutia. Kichwa cha hadithi kiwe mwanzo kabla ya kuanza kwa hadithi yenyewe. Maranyingi kichwa cha hadithi huandikwa kwa herufi kubwa au wino uliokozwa.

Mfano: KISA CHA CHONGO WATATUS

- **Mwanzo**

Maranyingi mwanzo wa hadithi huwa na namna maalumu. Mfano; “Hapo zamani za kale.....!

- **Mwendelezo**

Hii ndiyo sehemu kuu ya matukio ya hadithi nzima. Katika sehemu hii matukio ya hadithi hupangwa kwa mtiririko mzuri na wenye kuzingatia aya.

- **Mwisho**

Maranyingi hadithi za ngano humalizika kwa namna maalumu. Aghalabu mtunzi husema, “ Basi chongo wale walipata uwezo wa kututumia macho yao yote, wakaoa na wakaishi raha mustarehe”.

Mwisho wa hadithi ni lazima uwe katika aya.

- **Muundo au msuko;** ngano yapaswa kuwa na ploti au mpangilio rahisi wa matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho. Masimulizi yote yatolewe kwa kusisimua ili kuwawutia wasikilizaji.

- **Mandhari;** mtunzi wa ngano anapaswa kujenga mazingira ya wakati na mahali yanapotendeka matukio mbalimbali.

- **Matumizi ya lugha;** mtunzi wa ngano anapaswa kutumia lugha rahisi na ya kinathari lakini ya kuvutia iliyojaa methali, misemo, tamathali za semi, lugha ya picha na kadhalika.
- **Wahusika;** ngano huhitaji wahusika wa aina nyingi kama vile; wanyama, mimea, miungu na kadhalika.  
Ni muhimu wahusika watumiwe kikamilifu kukuza kisa au visa na kuitisha ujumbe.
- **Mbinu nyingine;** mtunzi wa ngano anaweza kutumia mbinu mbalimbali katika kukamilisha hadithi yake. Mbinu hizo ni kama vile:
  - \*Matumizi ya nyimbo
  - \*Matumizi ya dayolojia

### **Mfano wa hadithi ya ngano:**

#### **DEGE**

Hapo zamani za kale waliondokea mtu, mkewe na mtoto wao wa kiume. Watu hao walikuwa na maisha mazuri tu amabayo hayana hitaji lisilokidhiwa. Siku moja majira ya asubuhi sana, yule mtoto mwanamume alikuwa nje akicheza. Mara hiyo alimwona kipepeo mzuri mno, mwenye rangi mzomzo, zilizooana kwa urembo na ulimbo wa ajabu.

Yule mtoto akawa anajaribu kumkamata yule Kipepeo kwa kwa kuchupa na kumrukia kama Sungura na Zabibu. Alichupaaaa, akaruka huyoooo. Lakini kila akichupa na kuruka, utadhani waliagana na Kipepeo yule, kwani Kipepeo alichupa na kuruka. Mtoto alizidi kuchupa na kuruka, akiwa anamfuatia yule Kipepeo. Yakawa ni mashindano ya kuchupa na kuruka. Haooooooo! Msitu na nyika, msitu na nyika; hata kushtukia wako mbaliii! Mtoto hajui mbele wala nyuma, hajui pa kupata njia wala kupotelea. Mradi tu alijikuta yuko peke yake, kachoka taabani wa Shaabani, kiu imemkamata kijana, ulimi nje nje kama wa Mbwa. Na kipepeo naye ndo hivo, haonekani tena.

Basi bwana! Kijana wetu huyo alikaa chini ya mti ambao ulikuwa umeambatana na mwamba uliokuwa katikati ya njia kubwa. Akawa anawaza ya nyumbani, lakini afanyeje masikini wa watu. Na jua nalo ndo hivyo linakwenda kama lilivyopangiwa. Njaa imembana, na kiu kimemkamata; afanye nini?

Ghafla, kijana wetu akaona matone yadondokayo kutoka kwenye mwemba. Matone yakazidi kodondoka, makubwa hayoooo. Kijana akakurupuka huyooo! Mbio kama vile kamwona tena yule Kipepeo. Akaokota kifuu cha nazi, akayakinga yale matone. Akakinga weeee! Hata wakati maji yale yanakaribia kujaa, akaona ayanywe kuituliza ile kiu yake kali. Akaelekeza kifuu chenye maji mdomoni mwake. Lakini ghafla likaja dege kubwa hilo! Dege lisilokuwa na mfano. Mbawa zake zilikuwa zikipiga, na upopo karibu umwangushe kijana wetu. Hiloo, likapiga kile kifuu na kumwaga maji yooote! Halafu likajiendea zake likamwacha kijana ana haha kwa kiu na woga. Lakini kijana wetu hakukata tama. Alikinga mara ya pili; tena akawa ameshikilia kifuu imara zaidi ya mara ya kwanza. Lile dege likampokonya kifuu tena.

Mara ya tatu yalipotokea yale, kijana akaamua kwenda juu ya mwamba kuona kulikoni huko yanakotokea yale maji. Akapanda, akapanda, akapandaaa! Halafu juu kabisa ya ule mwamba, kijana akalikuta Joka! Joka Joka hasaaa! Limelala utadhani limekufa, ijapokuwa macho yake makunwa kama nazi yalikuwa yakigeuka geuka kama ya Kinyonga. Kijana hakulikaribia dude lile; bali pale akagundua yalikokuwa yanatoka yale maji. Domo la Joka lile lilikuwa wazi, na sumu ikatiririka kama maji mferejini hadi kule chini ya mwamba. Kijana mwili ulimsisimka, moyo ukamchachatika.

Ghafla lile dege likaja tena. Mara hii si kwa kasi kama mwanzo. Masikini kijana wetu! Kule nyumbani wazi wake wote wawili wa kukeni na wa kuumeni walikuwa wakikata roho kwa huzuni ya kumpoteza mtoto wao.

Lile dege likamjia yule mwanamume na kumchukua hangahanga, juu kwa juu. Likawa linampepea mwanamume yule asiungue jua. Lilipaaaaa. Halafu ghafla likaanza kushuka. Kijana mwanamume alipoangalia chini akajua kuwa karudishwa nyumbani kwao. Akafurahi!

### ➤ VIGANO

Ni hadithi zinazoelezea makosa au uovu wa watu fulani na kuelezea maadili yanayofaa. Maranyingi vigano hutumia methali, misemo au nahau kama msingi wa kutolea maadili kwa jamii.

Mfano; “**Samaki mkunje angali mbichi**”

#### **Kanuni za utunzi wa vigano**

Utunzi wa vigano huongozwa kwa kanuni zifuatzo:

- ❖ **Uteuzi wa anuani:** Maranyingi vigano hutumia methali, misemo au nahau kama msingi wa kutoa mafunzo.  
Mfano,- Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe
  - Samaki mkunje angali mbichi
- ❖ **Madhumuni:** Unapotunga ni muhimu kuzingatia madhumuni. Madhumuni huweza kuwa kukanya, kuelekeza, kuadibu au kufunza.
- ❖ **Maudhui:** Vigano hueleza hali, matendo bora na masahibu ya wahusika ili walioengwa wajifunze kutokana na makosa ya wahusika.
- ❖ **Fani:**  
Vipengele vya fani vinavyobainika katika vigano ni kama vifuatavyo:
  - **Msuko;** Vigano huwa ni rahisi na hujengwa kwenye kisa kimoja tu.
  - **Muundo;** Vigano huwa na muundo wa hadithi za kawaida ambazo hujumuisha mwanzo, mwendelezo na mwisho.
  - **Mandhari;** Masimulizi ya vigano hujifunga katika mazingira maalumu ya wakati na mahali.
  - **Wahusika;** Wahusika wanaotumiwa katika vigano huwa ni wanadamu au wanyama lakini wote hulenga kumuadilisha mwanadamu.
  - **Matumizi ya lugha;** Lugha inayotumiwa katika vigano ni lugha kama inayotumiwa na hadithi zingine. Lugha hii imejaa matumizi ya tamathali za semi, semi na mbinu mbalimbali za kisanaa.

**Mfano wa kigano:**

## **MTOTO UMLEAVYO NDIVYO AKUAVYO**

Siku moja Sheikh Ally alikwenda kuwatembelea wafungwa waliokuwa wamepata hukumu ya kifo. Mmoja wa wafungwa hao alikuwa na kisa cha kusikitisha cha kusimulia:

Jina langu ni Abdul. Nimekuwa jambazi la kuwanyang'anya watu mali zao kwa kutumia nguvu. Nimefanya kazi hii kwa muda mrefu. Hatimaye siku yangu ya arobaini imewadnia. Ninasikitika kusema kuwa wazazi wangu bila kukusudia hivyo walisaidia kujenga tabia ya wizi ndani yangu, tangu utotoni mwangu.

Nilipoingia darasa la kwanza, kama watoto wengine, sikuweza kutunza vitu vyangu. Kila siku, nilikuwa nikipoteza kalamu na kifutio changu. Wazazi wangu walinchapa na kunikemea vibaya sana. "Sikiliza Abdul, sisi wazazi wako usifikiri kuwa tuna kiwanda cha kalamu na vifutio. Hatuwezi kuendelea kununua kalamu na vifutio kila siku". Niliendelea kupoteza vifaa hivi, licha ya onyo na pigo kali nililolipata. Nilipotupiwa kalamu. Chukua hiyo kalamu, wewe mjinga! Ukiipoteza hiyo, usije hapa kutaka nyingine. Hatutakununulia! Kichwa kikubwa lakini huna akili! Umezaliwa na nani? Nani kakwambia pesa zinaokotwa kwenye jalala? Lakini sikupoteza makusudi, niliibwa! "Nilijitetea". "Kwani wewe tu ndiye unayeibwa? Wewe huwezi kuiba? Kila siku wimbo umekuwa huo huo; nimeibwa! Ukiibwa na wewe iba!" Mzazi alinikazania.

"Tatizo langu lilikuwa limetatuliwa". Nilihitaji ujasiri mkubwa sana kumwibia mwanafunzi mwenzangu kalamu. Mwanzioni ilinibidi kuketi kichakani kwa kuchelea kuchapwa na mwalimu kwa sababu ya kukosa kalamu. Mwalimu wa darasa alipiga ripoti kwa wazazi wangu kwamba, sikuhudhuria shulenii. Nilipowaambia wazazi wangu kwamba sikuenda kwa sababu sikuwa na kalamu nilipata adhabu isiyo kifani. Waliniuliza sababu ya kutowafahamisha kuhusu kupotea kwa kalamu ilihali walikuwa wamenionya nisiwapigie ripoti kuhusu kupotea kwa kifaa chochote. Hivyo ndivyo nilivyoanza kuwaibia wanafunzi wenzangu vitu vidogovidogo darasani. Kisha nilianza kuiba vitabu, saa na sweta za wenzangu na kufuta majina yao.

Wazazi wangu hawakujali kuniuliza nilipotoa vitu hivyo. Waliona kuwa nilikuwa ninawapunguzia mzigo wa ununuzi kila uthao. Nilipoingia shule ya sekondari, nilikuwa nimehitimu kuiba vitu vikubwa vya shule. Tuliwahi kuiba darubini zote za shule, kisha tukaiba runinga na kung'oa vichwa vyote vya simu katika ofisi ya mkuu wa shule. Tulikuwa tukivunja masanduku ya wanafunzi wenzetu na kuiba pesa na vitu vinginevyo vinavyouzika kiurahisi. Tuliiba pia godoro, blanketi! Na shuka za wanafunzi wenzetu na kuuza. Ikawa daima tuna pesa kama njugu.

Wanafunzi waliojua mienendo yetu tuliwatisha kwa kifo, endapo wangethubutu kutushitaki kwa mkuu wa shule. Mwisho wa wiki tulioroka shule na kwenda mjini kuhudhuria tamasha za densi. Lakini hatimaye tulipogunduliwa, tulifkishwa mahakamani. Tulifukuzwa shulenii kabisa, tukiwa kidato cha tatu.

"Baada ya kifungo chetu cha mwaka mmoja na nusu, tulikuwa tumehitimu kuwa majambazi hasa. Kifungo hiki kilitufanya kuwa sugu zaidi. Kwa muda wa miaka kumi iliyopita tumefanya kila aina ya ujambazi – tumeiba, tumeua, tumenajisi,

tumewanyang'anya watu mali kwa nguvu, mimi na rafiki yangu ambaye amepitia mkondo wa maisha kama wangu. Ninasikitika kusema kuwa, halikuwa kusudi langu kuongeza idadi ya majambazi katika taifa hili. Lakini wazazi wangu walichangia kwa kiasi kikubwa mimi kuwa jambazi.

Ninaposubiri siku yangu ya kifo, ninataka ulimwengu ujue kwamba, damu yangu itawaelekeea wazazi wangu. Hata hivyo, ninajilaumu mimi mwenyewe kwa kuwa nilikuwa nina hiari ya kuchagua baina ya ujambazi na maisha ya uadilifu. Ninatubu kwa Mungu na kwa walimwengu niliowadhulumu na kuyakatisha maisha yao. Sistahili msamaha duniani na akhera.

Hapo Abdul aliangua kilio cha kwikwi na kuangukia kifuani mwa sheikh Ally. Askari wa gereza alimchukua Abdul na kumkomelea ndani. Sheikh Ally alibakia akitikisa kichwa.

### ➤ **TARIHI/ VISAKALE**

Ni hadithi ambazo husimulia kuhusu matukio ya kihistoria. Matukio hayo yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni. Matukio hayo hujengwa kisanaa ili kuwavutia hadhira.

Maranyingi wahusika wake ni binadamu ila hujengewa uwezo mkubwa au mdogo kulingana na matukio yanayosimuliwa.

#### **Kanuni za utunzi wa tarihi**

Ili kutunga tarihi, mtunzi anapaswa kufuata kanuni zifuatazo:

- ❖ **Dhamira:** Mtunzi wa tarihi anapaswa kuweka dhamira ya kutunga tarihi yake. Dhamira ya tarihi huweza kuwajuza wanajamii, kuelimisha, kuburudisha au kuwapa watu kujitambulisha.
  - ❖ **Aina:** Mtunzi wa tarihi anapaswa kuamua aina ya tarihi ya kutunga. Tarihi yaweza kuhusu jamii, nchi, mji, kijiji au mtu.
  - ❖ **Maudhui:** Mtunzi wa tarihi anapaswa kupanga maudhui ya tarihi yake. Maudhui ya tarihi hutokana na majibu ya maswali yafuatayo;
- **Nini au nani anahusika?** Hapa mtunzi anapaswa kutaja jina la mtu, maumbile yake au sifa nyingine.
- **Kulitokea nini?** Mtunzi wa tarihi anapaswa kutoa maelezo kuhusu matukio na matendo muhimu.
- **Yalitokea lini?** Hapa mtunzi anapaswa kueleza muktadha wa wakati.
- **Yalitokea wapi?** Hapa mtunzi anapaswa kueleza mahali yalipotokea hayo matukio.
- **Yalimhusu nani?** Mtunzi wa tarihi anapaswa kueleza waathiriwa wa matukio hayo.
- **Kwa sababu gani?** Mtunzi wa tarihi anapaswa kueleza sababu za kutokea kwa matendo hayo.
- **Matendo yalikuwa na athari gani?** Mtunzi wa tarihi ni lazima aeleze sababu za kutokea kwa matendo hayo.

- ❖ **Fani:** Mtunzi wa tarihi hanabudi kutumia mbinu zifuatazo:
  - **Umbo;** Tarihi huwa na sehemu nne kama ngano. Yaani, utangulizi, mwanzo, mwendelezo na mwisho.
  - **Muundo:** Tarihi inahitaji kuwa na mtiririko rahisi na ploti yenyе matukio yanayohitilafiana lakini yenyе mvuto.
  - **Mandhari:** Mandhari hutolewa kwa ajili ya kujulisha mahali yalipotokea matukio hayo.
  - **Wahusika:** Katika tarihi yoyote huwa kuna wahusika mbalimbali. Maranyingi kuna mhusika shujaa anayeitwa JAGINA. Mhusika huyo anaweza kuwa mtu.
  - **Matumizi ya lugha:** Lugha ya tarihi huwa ni lugha ya kifasihi yenyе chuku nyingi inayoburudisha na kuibua hisia miongoni mwa watu.
  - **Mbinu nyngine:** Katika utungaji wa tarihi mbinu zinazotumika ni kama za ngano.
  
- ❖ **Kichwa:** Tarihi huwa na kichwa cha habari.

#### **Mfano wa tarihi:**

#### **NJAA NA MAAFA**

Siku moja waganga walimwenda mfalme Jaba Nene na kumwambia, “Ewe mtukufu mheshimiwa, mfalme wetu Jaba Nene! Sisi watumishi wako tumefikiwa na ndoto kwamba nchi yetu hii nzuri huenda ikakibiliwa na shida kubwa. Hii ni shida ya njaa na vita vikuu, maana maadui zetu wanajipanga kutushambulia hivi karibuni”.

Mfalme Jaba Nene aliwasikilza waganga kwa makini sana. Kisha alii nuka kwenye kitu chake cha enzi na akatamka. “Eeeyi, waganga wanchi hii nzuri yenyе mali tele !Eeeyi, waganga wa Undurubo! Je, mnataka tufanye nini ili kuzikinga shida hizo ambazo zimepatikana ndotoni?”

Mkuu wa waganga hawa alimwambia Mfalme Jaba Nene, “Eewee Mfalme mashuhuri wa Undurubo! Kile ambacho tunapaswa kufanya ni kutenda, na ni lazima tufanye tendo hivi sasa kabla mambo hayajaharibika zaidi. Sisi kama watumishi wako waaminifu tutakupa kila siri na utabiri wetu ulio sawa kabisa. Tumefikiwa ndotoni kwamba kuna majitu yanayoishi msituni yapata umbali wa kilomita mia tano kutoka hapa. Majitu haya ni hodari sana, tena yana uwezo wa kuangamiza dunia hii bila shida.”

Waganga walimweleza Mfalme Jaba Nene kwamba kile anachopaswa kukifanya ni kumchagua Amri Jeshi mkuu ambaye ni mtu hodari sana na shujaa kushinda wote. Walimweleza kwamba kazi ya huyo shujaa itakuwa ni kwenda kuyatafuta majitu haya. Akiyapata, ni lazima akate mkia wa jitu moja na kuuleta mbele ya Mfalme, na hapo shida na njaa pamoja na tishio la vita lingewaondoka wenyeji wa Undurubo.

Ijapokuwa mfalme Jaba Nene aliwasikiliza maneno haya kwa makini, lakini hakufanya vile alivyoagizwa na waganga hawa. “Aaah, hawa waganga wanajua nini. Siku zote kazi yao ni kujitafutia mlo tu, na kuuleta fitina nchini”.

Baada ya miaka michache tangu utabiri huo wa waganga kufanywa, nchi ya Undurubo ilianza kukabiliwa na njaa. Kulikuwa na hali mbaya ya Kiangazi. Mvua ilipotea kwa muda wa miaka miwili mfululizo. Wanyama wengi kama vile n'gombe, farasi, mbuzi, kondoo na hata kuku walikufa. Hapakuwa na mimea yoyote, na raia wengi walishikwa na njaa kali mno.

Nguvu za nchi ya Undurubo zilianza kupunguka, na majeshi ya nchi hayakuweza kupigana kishujaa tena mipakani na waasi, ambao walikuwa wakiishambulia kutoka nchi za jirani.

Maadui kutoka nchi za Ujimbi na Ulegui waliteka sehemu kubwa ya nchi ya Undurubo. Sehemu hizo zilizotekwa zilikuwa na ardhi yenyе rutuba nyingi. Jambo hili lilileta wasiwasi mwangi nchini. Mamia wa raia walimwendea Mfalme, wakamsihi ili afanye vile waganga walivyomshauri, lakini hawakujali. Kwa sababu ya ukosefu wa chakula, jeshi la Undurubo hawakuweza kupigana tena kwa ushujaa na wanajeshi wengi walitoroka.

Wakuu wa dini mbalimbali waliiomba miungu ya kuiga ili wapate mvua lakini wapi! Hali ya Kiangazi ilizidi kuwa mbaya kuliko vile iliviyopata kuonekana mbeleni. Mfalme Jaba Nene alikuwa na farasi wake aliyempenda sana hata kuliko wanadamu. Farasi huyo wa kifalme alikuwa akiitwa Duma. Farasi Duma alianza kukonda, na hatimaye alikufa kwa njaa. Kifo cha Duma kilimtisha sana Mfalme Jaba Nene. Alianza kufikiria yale ambayo aliambiwa na waganga.

Kwa haraka, Mfalme alitoa tangazo kwa wakuu wa ulinzi akiwaamuru wakusanye waganga wote nchini na kuapeleka kwake baada ya masaa ishirini na manne. Wakuu wa jeshi walifanya vile walivoagizwa, na wakishirikiana na idara ya ulinzi waliwanasa waganga wote na kuapeleka mbele ya Mfalme Jaba Nene siku iliyofuatia tangazo hilo.

## ➤ VISASILI

Ni hadithi ambazo husimulia mambo yanayohusiana na maumbile ya watu, miti, wanyama na kadhalika. Ni hadithi zinazoelezea asili ya viumbe wenye uhai au wasiokuwa na uhai.

### **Kanuni za utunzi wa visasili**

- ❖ **Dhamira ya kuelezea asili ya jambo:** Mtunzi anapaswa kuelezea dhamira yake iliyomfanya atunge kisasili hicho. Dhamira hiyo inaweza kuwa kuthibitisha, kufahamisha au kuhatarisha jambo.
- ❖ **Kuteua jambo la kutungia kisasili:** Visasili havisimuliwi kulingana na ukweli wa kihistoria wala kisayansi, bali hutungwa kulingana na imani za watu wanaohusika. Mtunzi wa visasili anapaswa kufanya uchunguzi na utafiti wa kuteua jambo analolitungia kisasili. Mambo ya kutungia visasili ni kama vile wanyama na mimea, mwanzo wa maumbile kama vile maziwa na milima na asili ya binadamu kama vile kabilia, ukoo na tabia.

- ❖ **Maudhui**: Maudhui ya visasili hujumuisha jina la kinachohusika, mahali kinapotokea, mazingira, matukio, mabadiliko, sababu za mabadiliko na hali ya sasa.
- ❖ **Fani**: Vipengele vya kuzingatia kwa mtunzi wa visasili katika fani ni kama vifuatavyo:
  - **Umbo**; visasili huwa na sehemu kama za ngano
  - **Muundo**; visasili huwa na ploti rahisi kuanzia mwanzo hadi mwisho.
  - **Muktadha**; Ni muhimu mtunzi ajenge muktadha wa umbali kimasafa na kiwakati. Mfano, “Hapo zamani za kale....”
- ❖ **Wahusika**: Wahusika huwa ni mtu, jamii au kitu.
- ❖ **Matumizi ya lugha**: Lugha ya kutungia visasili huwa ni ya mantiki inayoelezea maumbile na mazingira kikamilifu. Lugha hii hujengwa matumizi ya methali, misemo na tamathali mbalimbali za semi.
- ❖ **Mbinu nyingine za kisanaa**: Mtunzi anaweza kutumia mbinu nyingine za kisanaa kama vile nyimbo, majigambo, miujiza na kadhalika.

#### **Mfano wa Kisasili:**

#### **KISA CHA KIBOKO**

Hapo zamani za kale palikuwa na kundi kubwa la wanyama. Kundi hilo lilikuwa likiongozwa na mfalme wao aliyekuwa akiitwa Simba. Mfalme wao alikuwa na ujasiri sana na alikuwa akipendwa na wanyama wote. Kiboko alikuwa ni mnyama mwenye manyoya mengi sana.

Siku moja Kiboko alikuwa akihisi baridi, akaenda kwa rafiki zake Tembo na Ngedere ambao walikuwa wakiota moto, nao akajiunga nao wakiwa wanaota moto. Muda ulienda sana, Tembo na Ngedere waliondoka kwenda kulala, alibaki Kiboko peke yake akiendelea kuota moto kwani alikuwa akihisi baridi sana. Kiboko alizidi kuongeza kuni ili moto uendelee kuwaka.

Baada ya Kiboko kuota moto kwa muda mrefu alipitiwa na usingizi. Kumbe! Upopo mkali ulikuwa ukivuma, ule upopo ulitoa cheche ambazo zilimfikia Kiboko katika mwili wake na manyoya yake kuanza kuwaka mithili ya kichaka kilichotupiwa njiti za kiberiti. Kiboko alipiga kelele huku akikimbilia mtoni; na alipofika mtoni alijitupa kwenye maji na ule moto ukazima. Wanyama wenzake walipoona hatokezi kwenye maji walidhani amekufa.

Baada ya muda mrefu, Kiboko alitokea akiwa hana unyoya hata mmoja, na ngozi yake kuwa nyororo kuliko kawaida. Wanyama wenzake walifurahi kumuona yupo hai, Kiboko alijihisi kama yupo uchi na akamuomba mfalme aendelee kukaa mtoni. Mfalme alikataa kwa kumwambia, “Ukikaa mtoni utakula samaki wetu”. Kiboko alimwambia mfalme

kuwa hangeweza kufanya hivyo. Kiboko aliendelea kumwambia mfalme, “Sitatanya hivyo mfalme, ili kukuhakikishia kwamba sitafanya hivyo, kila nikitoka kwenye maji nitaachama mdomo wangu ili kukuonesha kama nimekula samaki au la.” Ndipo mfalme alimruhusu kuishi katika maji hapo mtoni na wanyama wengine walikubali”.

Ndiyo maana mpaka leo hii kiboko hana manyoya na anaishi mtoni na kila anapoibuka kutoka mtoni lazima aachame mdomo wake.

### ➤ SOGA

Ni hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli. Wahusika wake ni wa kubuni.

Soga hukejeli hali inayohalisika. Wahusika hupewa majina ya watu walio katika mazingira hayo. Soga husema ukweli unaoumiza lakini ukweli huo hujengwa na kichekesho ili kupunguza ukali wa ukweli huo.

Soga hujengwa juu ya tukio moja ambalo hukusudiwa kuchekesha kwa kubeza au kukejeli.

### **Mfano wa soga**

Jamani tujiangalie, mambo mengi vichekesho. Bwana Nasoro mwaka juzi alipata cheo. Kapewa ofisi ya baridi, wahudumu kabakaba na gari la mneso lenye dereva kijana. Basi Nasoro akawa anaingia kila baa, kila hoteli kutangaza cheo chake. Kila akichapa bia na kuku basi, Kiingereza kinamtoka “Remember am Boss!” Mashabiki wanamwitikia kwa shangilio kwa kuwa bia anawapa. Basi bichwa likamvimbba kama boga. Januari mwaka huu wakamng’aza maana shirika linadidimia yeye anainukia. Basi wamemtoa pale yupo wizarani anapiga miayo.

### Vyanzo vyat hadithi

- (i) **Historia na mazingira ya jamii.** Historian a mazingira ya jamii husababisha kuzaliwa kwa hadithi mbalimbali. Mfano hadithi za mwanzo za ngano zilizuka wakati mtu anapigana na mazingira yake mwenyewe.
- (ii) **Mabadiliko ya kijamii.** Mabadiliko ya kijamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yanaweza kusababisha kuzuka kwa hadithi. Mabadiliko hayo yanaweza kueleza matukio hayo na athari zake kwa jamii inayohusiska.
- (iii) **Shughuli mbalimbali za kijamii.** Shughuli za kijamii kama vile, harusi, kilio jando na unyago, matambiko na kadhalika huweza kuzalisha hadithi. Hii hutokeea pindi watu wanaposimulia mambo hayo kwa vizazi vyat sasa.

### (B) USHAIRI

Ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno yenye muwala, lugha ya picha katika kueleza jambo fulani kuhusu jamii.

#### Au


Ni fungu linalojumuisha tungo zote zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalumu. Mapigo hayo yanaweza kupangwa kwa kwa muwala wa urari wa vina na mizani.

### **VIPERA VYA USHAIRI**

Ushairi hujengwa kwa vipera vifuatavyo:

➤ Mashairi

- Utenzi
- Ngonjera
- Majigambo
- Nyimbo
- Maghani



➤ **MASHAIRI**

Ni aina ya ushairi ambao huwa na maneno yenyε ruwaza mahsusι ya silabi na lugha ya mkato kwa lengo la kutoa ujumbe fulani kwa jamii.

Mashairi ni sehemu tu ya ushairi ambayo hueleza kwa ufupi mambo fulani kuhusu binadamu na mazingira yake.

**Aina za mashairi**

Kimtindo, mashairi yapo ya aina mbili (2)

- (a) Mashairi ya kimapokeo
- (b) Mashairi ya kisasa

### (a) **Mashairi ya kimapokeo**

Ni mashairi yanayofuata urari wa vina na mizani. Mashairi ya kimapokeo hujulikana kama mashairi ya jadi.

Mashairi haya huitwa ya kimapokeo kwa sababu ndiyo yalikuwa mashairi ya kwanza kuanza kutungwa katika ulimwengu huu wa fasihi.

### **Kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo**

Mashairi ya kimapokeo hutungwa kwa kuzingatia kanuni zifuatazo:

- **Vina:** Vina ni silabi zinazofanana sauti zinazojitokeza katikati na mwishoni mwa mshororo/ mstari wa shairi.
- **Ikumbukwe;** vina ni silabi na wala si herufi. Ingawa herufi inaweza kuwa silabi.

**Mfano:** Pale ung'oapo **jino**, uwazi unabakia,  
Sura ya huzuni **mno**, tena ya kufurahia,  
Nataka unga **mkono**, penye nia pana njia,  
Ishirini moja **tano**, maua yangu chanua.

\*Katika ubeti huo wa shairi vina na “**no**” na “**a**”

### **Aina za vina**

Kuna aina mbili za vina. Kuna vina vya kati na vina vya mwisho

- **Vina vya kati;** ni vina vinavyopatikana katikati mwa mshororo wa shairi. Katika ubeti huo hapo juu vina vya kati ni “**no**”
- **Vina vya mwisho;** ni vina vinavyopatikana mwishoni mwa mshororo. Katika ubeti huo hapo juu vina vya mwisho ni “**a**”

**Kumbuka:** Mtunzi wa shairi la kimapokeo ni lazima azingatie urari wa vina.

Vina sio lazima kufanana katika beti zote za mashairi. Kila ubeti unawenza kuwa na vina vyake kutegeMEA utashi wa mtunzi.

- **Mizani:** Ni jumla ya silabi zilizopo katika kila mstari wa ubeti. Katika ushairi hizi ndizo ziletazo urari wa mapigo, kwani kila mstari unatakiwa uwe na mizani sawa na mistari mingine. Kwa kawaida shairi la kimapokeo huwa na mizani kumi na sita (16) yaani nusu mstari mizani minane na nusu mstari mwengine mizani minane.

Mfano; **Pa – le-u- ng'o- a- po-ji-no, u-wa-zi-u-na-ba-ki-**a****  
 1 2 3 4 5 6 7 8 1 2 3 4 5 6 7 8

- **Ubeti:** Hiki ni kifungu chenye kuleta maana kamili katika jumla ya vifungu vilivyomo katika utungo. Ubeti hubeba wazo kuu mojawapo katika ushairi. Ubeti wa shairi huundwa kwa idadi ya mistari kadhaa. Ubeti huweza kuundwa kwa:
  - Mstari mmoja, ubeti huu huitwa **TAMOLITHA**
  - Mistari miwili, ubeti huu huitwa **TATHNIA**
  - Mistari mitatu, ubeti huu huitwa **TATHLITHA**
  - Mistari minne, ubeti huu huitwa **TARBIA**
  - Mistari mitano, ubeti huu huitwa **TAKHMISA**

- Mistari sita na kuendelea, ubeti huu huitwa **SABILIA**

Idadi hiyo ya mistari katika ushairi huitwa MUUNDO. Maranyingi mashairi ya kimapokeo huwa na muundo wa **TARBIA**.

- **Kituo:** Huu ni mstari wa mwisho katika kila ubeti wa shairi. Kituo huweza kuwa kimalizio au kiini.

#### **Aina za kituo**

- **Kituo bahari;** ni aina ya kituo ambacho hujirudiarudia katika kila ubeti wa shairi.
- **Kituo kimalizio /mwisho;** ni aina ya kituo ambacho hujitokeza katika kila ubeti wa shairi.
- **Kipande:** Hiki ni kisehemu kimojawapo katika vijisehemu viwili au zaidi vya kila mstari (kwa tungo zenyewe kugawanyika katika sehemu mbili au zaidi katika kila mstari)
- **Utoshelezi:** Shairi la Kiswahili, kila ubeti unapaswa kujitosheleza bila kutegemea ubeti mwingine.
- **Muwala:** Shairi lazima liwe na muwala, yaani ufuatanisho wa habari kutoka ubeti mmoja kwenda mwingine. Shairi lisilokuwa na muwa unaweza kulikuta ubeti wa tatu unakuwa wa kwanza wa pili unakuwa wa nne.
- **Kuwa na maana:** Shairi lisifuate kanuni tu, bali linapaswa kuwa na maana. Shairi lazima liwe na maana kamili ili msikilizaji aweze kupata ujumbe.

#### **Mambo yanayolifanya shairi kuwa bora na zuri**

- **Kichwa:** Shairi ni muhimu liwe na kichwa. Shairi ambalo halina kichwa linapungua utamu wake.
- **Kutorudia maneno:** Shairi linaharibika na kupungua uzuri wake ikiwa mtunzi atarudia rudia maneno.
- **Kutochanganya dhamira:** Kuchanganya dhamira mbili au tatu katika shairi moja ni kuharibu shairi. Ni jambo zuri katika shairi litatumia dhamira moja ili hadhira upate ujumbe unaoelewewa.

#### **Uhuru wa Mshairi**

Mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa shairi. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lizingatie umbo fulani. Zifuatazo ni njia mbalimbali ambazo mtunzi wa shairi anaweza kutumia kuonyesha uhuru wake.

1. **Inkisari** - kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo.  
mfano: kubadilisha **nimeona aliyenipenda** kuwa **meona aliyenipenda**.

2. **Mazda** - kuongeza silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo.  
mfano: *afya ukijaliwa kuwa afya ukijaliwa* .
3. **Tabdila** - kubadilisha silabi ya mwisho ili kustawazisha urari wa vina katika kipande bila kuathiri mizani.  
mfano: *yahuzunisha dunia kuwa yahuzunisha duniya* .
4. **Kuboronga Sarufi** -ni mbinu ya kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi.  
mfano: *siku hiyo ikifika kuwa ikifika hiyo siku* .
5. **Utohozi** - Kuswahlisha Maneno - Wakati mwininge mshairi anaweza kubadilisha neno la lugha nyingine litamkike kwa Kiswahili ili kudumisha mdundo wa kishairi na pia kupata neno mwafaka litakalotimiza arudhi za kiushairi.  
mfano: tukapata intaneti badala ya tukapata 'internet' ama mtandao wa tarakilishi.

#### (b) Mashairi ya kisasa

Ni aina ya mashairi yasiyofuata urari wa vina na mizani. Mashairi ya kisasa pia hujulikana kama mashairi huru/Kimapingiti /MASIVINA.

Kiutunzi mashairi haya huwa hayana kabisa ulinganifu wa vina na mizani ukilinganisha na mashairi ya kimapokeo.

Mashairi haya hufuata mambo mengine kama vili:

- Beti
- Utoshelezi
- Muwala
- Kuwa na maana
- Kichwa na kadhalika

#### ➤ UTENZI

Ni aina ya ushairi ambao hutoa maelezo au masimulizi mrefu juu ya jambo. Utensi huweza kuelezea wasifu wa mtu au watu fulani.

#### **Kanuni za utunzi wa tenzi**

Mtunzi wa tenzi hanabudi kuzingatia kanuni zifuatazo:

- **Maudhui:** Tenzi huelezea matukio yanayotokea au yaliyotokea katika jamii.  
Tenzi hujihusisha na matukio ya kisiasa, kivita, kihistoria na kishujaa.  
Tenzi pia husimulia mambo ya furaha, misiba, wasifu wa watu na hata mawaidha.

Ni muhimu mtunzi wa tenzi atue maudhui baada ya kufanya uchunguzi kutegemea uzito na umuhimu wa suala la kutungia utenzi kwa jamii.

**Mfano;** Umuhimu wa katiba mpya, Watoto wa mitaani na kadhalika.

- **Fani:** Mtunzi wa tenzi hanabudi kuzingatia vigezo vya fani vinavyohusiana na tenzi; Vigezo hivyo :
  - (a) **Beti:** Kwa kawaida tenzi huwa na beti nyingi lakini urefu wake utategemea utashi wa mwandishi. Kila ubeti ubebe ujumbe ambao utachangia maana ya utenzi mzima.
  - (b) **Mistari:** Kila ubeti una mistari minne. Yaani muundo wa Tarbia
  - (c) **Mizani:** Mistari ya tenzi huwa na mizani (6) hadi (12) kwa kila mstari. Hata hivyo kila utenzi lazima udumishe idadi ya mizani. Maranyingi tenzi huwa na mizani minane (8). Yaani nusu mstari wa shairi la kimapokeo.
  - (d) **Vina:** Tenzi huwa na urari wa vina. Vina hivyo huwa ni vya nje tu. Mstari mitatu ya mwanzo huwa na vina vyenye urari sawa, na mstari wa mwisho wa kila ubeti huwa na kina tofauti. Na kina hiki huwa hakibadiliki katika beti zote tokea mwanzo hadi mwisho. Kina hiki huwa BAHARI.
- **Matumizi ya lugha:** Mtunzi anashauriwa atumie lugha ya Kiswahili iliyosheheni maneno ya mkato, mpangilio maalumu wa maneno yanayotoa picha na kadhalika.
- **Wahusika:** Tenzi huzungumzia mambo kuhusu wahusika maalumu. Yapasa sifa hizo zilitokeze.
- **Kichwa:** Ni muhimu mtunzi atue kichwa kinachoambatana na kiini cha utenzi.

**Mfano wa utenzi:**

**UMUHIMU WA MISITU**

Utenzi nawatungia,  
Mazuri kuwaambia,  
Misitu kujitunzia,  
Faida kujipatia.

Dawa inatupatia,  
Wagonjwa kujitibia,  
Maisha yaendelea,  
Watu wanafurahia.

Matunda yasaidia,  
Njaa tunaitatua,  
Fukara wafurahia,  
Maisha kuendelea.

Utenzi naumaliza,  
Mengi nimeyaeleza,  
Naamini tunaweza,  
Misitu kujitunzia.

**Swali: Fafanua tofauti nne (4) zilizopo kati ya utenzi na mashairi ya kimapokeo.**

➤ **NGONJERA**

Ni tungo za kishairi ambazo huwa na majibizano baina ya wahusika. Ngonjera huwa na muundo wa mashairi ya kimapokeo. Ngonjera huhusisha malumbano au kujibiza kwa wahusika kwa lengo la kutoa ujumbe kwa hadhira.

**Kanuni za utenzi wa ngonjera**

Tunapotunga ngonjera, tunapaswa kuzingatia kanuni zifuatazo:

- (a) **Kuteua mada:** Mtunzi wa ngonjera anapaswa kuteua mada aliyoikusudia kuwasilisha kwa hadhira.
- (b) **Kuweka dhamira:** Mtunzi wa ngonjera anapaswa kuweka dhamira yaani wazo kuu la mtunzi. Wazo hilo linaweza kuwa kutatua tatizo, kufafanua jambo, kuondoa utata na kadhalika.
- (c) **Kuteua maudhui:** Ni muhimu mtunzi achague hoja ambazo wahusika watatoa ili kuchangia suluhisho kuhusu mada. Hoja hizo ni lazima ziweze kuelimisha na kufahamisha wasomaji au wasikilizaji.

**Fani katika ngonjera**

Kama ilivyo katika utenzi wa mashairi kwa ujumla. Mtunzi wa ngonjera anapaswa kutumia fani zifuatazi:

- (a) **Mtindo:** Mtunzi wa ngonjera anapaswa kutumia mtindo wa mashairi ya kimapokeo
- (b) **Muundo:** Mtunzi anapaswa kutumia muundo mzima wa mashairi ya kimapokeo katika utungaji wake.
- (c) **Mandhari:** Mtunzi anapaswa kuteua mandhari itakayoendana na kile anachokijadili. Mfano – Mada ni kilimo, mandhari ni lazima yaendane na ukulima.
- (d) **Wahusika:** Katika kutunga ngonjera mtunzi anaweza kutumia wahusika wawili au zaidi au makundi mawili au zaidi. Kundi hilo linaweza kuwa kati ya raia na watawala.  
Kwa kawaida mhusika mmoja husema jambo moja kwa ubeti mmoja au zaidi na mhusika mwengine hujibu au huendeleza. Mwishoni mwa ngonjera wahusika hao hukubaliana na kuwa kitu kimoja.
- (e) **Matumizi ya lugha:** Mtunzi wa ngonjera anapaswa kutumia lugha ya kishairi. Hii hujumuisha matumizi ya lugha ya mkato, maneno teule, matumizi ya lugha ya picha, matumizi ya methali, misemo na tamathali mbalimbali za semi.

**Mfano wa ngojera:**

**Kaka:** Kusoma nilikosoma, nambiya sipati kazi,  
Yapata mwaka mzima, nategemea shangazi,  
Wasiojua husema, sababu sina ujuzi,  
Huo uhaba wa kazi, mesababishwa na wake.

**Dada:** Mbona watuingilia, kaka acha ubaguzi,

Likukeralo twambia, tulijue waziwazi,  
Au unalochukia, ni wake kufanya kazi?  
Mambo ya kisiku hizi, watu ni bega kwa bega.

### ➤ MAJIGAMBO

Ni masimulizi ya kujisifu kwa mtu kuhusu matendo ya aliyoyatenda katika maisha yake. Majigambo hutolewa kwa lugha ya kishairi na masimulizi yake huambatana na matendo ya anayejigamba.

Matendo hayo yanaweza kuwa ni kushinda vita, kuua adui na kadhalika.

#### **Kanuni za utunzi wa majigambo**

Katika kutunga majigambo, mtunzi anapaswa kuzingatia kanuni zifuatazo:

- (a) **Kuteua tendo la kutungia majigambo:** Mtunzi wa majigambo anapaswa kuteua tendo ambalo atalitungia najigambo yake. Maranyingi tendo hilo linapaswa kuwa la kishujaa na kijasiri. Matendo hayo ni:
- Kushinda mitihani
  - Kuokoa maisha
  - Kutetea haki za watu na kadhalika.
- Ni muhimu mtunzi atuee tendo la kutungia majigambo kutegemea uzito wake, upya wake, mazingira na hadhira.
- (b) **Maudhui:** Maudhui katika majigambo hutegemea urefu wa majigambo kwa hadhira, muda na mazingira. Hata hivyo mambo muhimu ya kutaja ni:
- (i) **Jina;** Kwa kawaida jina linaweza kuwa ni la kweli, la kubuni au lakabu.  
Mfano; Mimi ni Chuma! Mimi ni Jabali!
  - (ii) **Asili ya majigambo;** Mtu anayejigamba anapaswa kueleza asili ya kujigmba.  
Asili huweza kuwa ni kabilia, ukoo, jamii na kadhalika.
  - (iii) **Matendo;** Mtu anayejigamba anaweza kueleza tendo moja au msururu wa matendo aliyoyatenda. Ni muhimu pia kueleza wakati mahali na sababu za matendo.  
Mfano; Kuua Simba.
  - (iv) **Matokeo;** Maranyingi mtu anayejigamba huelezea matokeo ya matendo yake ambayo huwa ni ushindi kwake na fahari kwake lakini madhara, hasara na fedheha kwa mahasidi au maadui wake.
  - (v) **Matumaini;** Hapa mtunzi wa majigambo anapaswa kuonesha matumaini ya kuendelea na ushujaa siku za usoni.

- (c) **Fani:** hizi ni mbinu ambazo mtunzi wa majigambo anapaswa kutumia wakati wa kutunga majigambo yake. Mbinu hizo ni;

- (i) **Mtindo;** Mtunzi wa majigambo anapaswa kutumia mtindo wa kuficha jambo, kufumba au taswira nzito.  
Mfano – Badala ya kujisifu jinsi alivyookoa majeeruhi katika ajali ya daladala anaweza kusimulia jinsi alivyowaokoa watu waliopata ajali baharini.

(ii) **Muundo;** Kwa kawaida majigambo huwa na muundo wa kishairi lakini wenye mwanzo, mwendelezo na mwisho. Kwahiylo, mtunzi wa majigambo anapaswa kuweka:

- Kichwa cha majigambo
- Beti
- Lugha ya kishairi
- Alama za kuuliza, alama za mshangao.

(iii) **Wahusika;** Wahusika wa majigambo ni mijigambi mwenyewe na wengine alioingiliana nao katika matukio fulani.

(iv) **Matumizi ya lugha;** Lugha inayotumiwa ni ya kishairi inayoambatana na misemo, nahau, methali, taswira na tamathali mbalimbali za semi.

- Mtu anayejigamba anapaswa kutumia zaidi nafsi ya kwanza kujirejerea na nafsi zingine kuwarejerea wahusika wengine.

(v) **Mandhari;** Mtunzi anapaswa aeleze mazingira yanamotokea matendo. Mazingira yanaweza kuwa misitu, mtaa, ukumbi, uwanja na kadhalika.

### **Mfano wa majigambo:**

#### **MIMI NI JABALI**

Mimi ni Jabali lizualo tufani kwa kiganja,  
Kifua changu hata radi haipenyi,  
Yangu si ngozi ya kawaida,  
Vigumba vyta mikuki huvunjika vikigonga,  
Hata kimbunga hutoroka kinionapo,  
Hakuna ajuaye asili yangu,  
Hakuna awezaye kutabiri hatma yangu  
Apingae athubutu ajitokeze!

#### **➤ NYIMBO**

Ni tungo za ushairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Wimbo ni kila kinachoimbwa.

Mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ni:

- Muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji
- Muziki wa ala (kama upo)
- Matini au maneno yanayoimbwa
- Muktadha unaofungamana na wimbo huo. Mfano, sherehe, ibada, kilio, harus na kadhalika.

### **Tanzu za nyimbo**

Baadhi ya tanzu za nyimbo zinazojulikana sana hapa Tanzania ni:

- **Tumbuizo;** ni nyimbo za furaha ziimbwazo kufurahisha watu kwenye matukio mbalimbali. Mfano; ngomani au harusini.
- **Bembea;** ni nyimbo za kubembelezea watoto.
- **Kimai;** ni nyimbo zinazohusu shughuli za baharini
- **Mbolezi;** ni nyimbo za kilio au maombolezo
- **Nyiso;** ni nyimbo za jando na unyago
- **Wawe;** ni nyimbo za kilimo
- **Tendi;** ni nyimbo za kusifu mashujaa
- **Kongozi;** ni nyimbo za kuaga mwaka
- Nyimbo za vita
- Nyimbo za taifa
- Nyimbo za uwindaji na kadhalika.

### **Dhima ya nyimbo katika jamii**

- (a) Hutumika kuhifadhi matukio muhimu ya kihistoria.
- (b) Hutumika kama nyenzo muhimu ya kuitishia utamaduni wa jamii fulani.
- (c) Huweza kutumiwa kama burudani.
- (d) Hutumika katika kuelimisha jamii.
- (e) Hujenga umoja na mshikamano.

### ➤ **MAGHANI**

Ni ushairi unaotolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. Maghani yapo ya aina mbili(2)

- (a)Maghani ya kawaida
- (b)Maghani ya masimulizi

#### **(a) Maghani ya kawaida**

Haya ni maghani ambayo huingia fani mbalimbali za fasihi simulizi. Mfano, ushairi wa mapenzi, siasa, maombolezo kazi, dini na kadhalika.

#### **(b) Maghani ya masimulizi**

Hizi ni ghani zinazotambwa ili kusimulia hadithi, historia au tukio fulani na ambazo maranyingi huambatana na muziki wa ala. Mtambaji wa ghani hizi huitwa Yeli au Manju na kwa kawaida huwa ni bingwa wa kupiga ala fulani ya muziki. Kwa hapa Tanzania ala hizo ni kama vile; zeze, marimba, ngoma na njuga.

### **Sifa za ghani**

- Ni tungo za kishairi.
- Husimulia hadithi au tukio fulani kwa kirefu.
- Hutungwa papo kwa papo wakati wa utongoaji.

### **(C) SEMI**


Ni fungu la tungo la fasihi simulizi ambazo ni fupifupi zenye kutumia picha tamathali za semi na ishara. Aghalabu ni mafumbo yanayokusudiwa kubeba maudhui yenye maana zinazofuatana na ibara mbalimbali za matumizi.

- Mfano; - Haraka haraka haina baraka.  
- Uzi mwembamba umefunga dume kubwa.  
- Ana mkono wa birika.

### **Vipera vya semi**

Semi huundwa kwa vipera vifuatavyo;

- Methali
- Vitendawili
- Misemo
- Nahau
- Mizungu
- Lakabu
- Mafumbo



## ➤ **METHALI**

Ni semi fupifupi zenyе kueleza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na uzoefu wa kijamii. Maranyingi mawazo hayo huelenza kwa kutumia tamathali hasa sitiari na mafumbo.

Mfano; - Kivuli cha fimbo hakimfichi mtu juu.

- Mchimba kisima huingia mwenyewe
- Ukiona zinduna ambari iko nyuma
- Waarabu wa pemba wanajuana kwa vilemba
- MBAazi ukikosa maua husingizia juu.

### **Fani katika methali**

Methali huundwa kwa vipengele mbalimbali vya fani. Vipengele hivyo ni;

- **Muundo;** Methali nyingi huwa na muundo wa sehemu mbili: Sehemu ya kwanza huanzisha wazo fulani na sehemu ya pili hulikanusha au hulikamilisha wazo hilo.

Mfano: -Jicho la mkata halioni / likiona haliongozi

- Mwenda tezi na omo / marejeo ngamani.
- Jino la pembe / si dawa ya pengo.

Sehemu ya kwanza kila wakati huwa ndefu kuliko sehemu ya pili. Urefu huo husababishwa na kuwa chanzo chake methali. Sehemu ya pili ni fupi kuliko sehemu ya kwanza. Hapa ndipo kwenye matokeo yaliyoelezwa katika sehemu ya kwanza.

- **Matumizi ya lugha;** Methali hujengwa matumizi mbalimbali ya tamathali za semi.

Methali nyingi huangukia katika mafungu yafuatayo ya tamathali za semi:

#### **Sitiari.**

Mfano: - Mgeni ni kuku mweupe

- Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa.

#### **Kejeli**

Mfano: - Ganda la muwa jana chungu kaona kivuno

- Uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti.

#### **Msisitizo**

Mfano: - Hayawi, hayawi, huwa.

- Hauchi, hauchi, huwa.

#### **Tashihisi**

Mfano: - Kiburi si maungwana.

- Siri ya mtungi aijuaye kata.

#### **Tashibiha**

Mfano: - Kawaida ni kama sheria

- Jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza.

### **Mbinu nyingine za Kisanaa**

#### **Onomatopea (Tanakali sauti)**

Mfano: - Chururu si ndo! Ndo! Ndo!

- Bandu! Bandu! Huisha gogo!

#### **Takriri**

Mfano: - Mtoto wa nyoka ni nyoka  
- Asiyejua maana, haambiwi maana.

#### **Maswali**

Mfano: - Pilipili usizozila zakuwashia nini?  
- Umekuwa bata akili kwa watoto?

#### **Mchezo wa maneno**

Mfano: - Pema usijapo pema, ukipema si pema tena.  
- Ukiiona neno usiseme neno, ukisema neon utapatwa na neno.

### **Picha na taswira katika methali**

Sifa muhimu ya methali ni kule kujenga picha au taswira ambazo huchorwa katika mazingira. Picha hizo zinaweza kuhusu wanyama, ndege, wadudu, samani, mazimwi na kadhalika.

#### **Picha za wanyama**

Mfano: - Paka akiondoka panya hutawala  
- Mzoea punda hapandi farasi.

#### **Picha za ndege**

Mfano: -Kuku mwenye watoto halengwi jiwe.  
-Kunguru mwoga hukimbiza mbawa zake.

#### **Picha za wadudu**

Mfano: - Maji ya kifuu ni bahari ya chungu.  
- Mtupa jongoo hutupa na mti wake.

#### **Picha za samani**

Mfano: - Kitanda usicholalia hujui kunguni wake.  
- Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.

- **Mazingira;** methali hufuatana na mazingira ya watu pamoja na silika, tamaduni na itikadi zao. Si rahisi kwa mtu kupata uzito wa maana au jibu au dhana ya picha za maneno yaliyotumika katika methali iwapo mtu huyo ana asili ya mahali methali ilipozaliwa.

### **Maudhui katika methali**

Katika maudhui tunaangalia jinsi methali inavyojishughulisha katika kuonesha silka, itikadi, utamaduni, tabia, uchumi, siasa, na uhusiano wa matabaka. Thamani ya methali ni ule ujumbe utolewao na utanzu katika kuielekeza jamii.

Methali nyingi hushughulikia mazingira yanayowazunguka watu, na kwa kawaida huchunguza maisha ya kawaida ya binadamu na mazingira yake. Kwahiyio basi, maudhui ya methali hutofautiana kutoka jamii na jamii kufuatana na mazingira na mahitaji ya jamii hizo. Maudhui ya utanzu huu huathiriwa pia na kazi ama dhima ya methali inayohusika. Methali ina matumizi mengi kwa jamii inayohusika. Matumizi hayo ni kama:

## **Kuelimisha**

Mfano: “**Mali bila daftari hupotea bila habari**” methali hii huelimisha wanajamii umuhimu wa kuweka kumbukumbu za mali zao hasa katika maandishi.

## **Kuburudisha**

Kama kiburudisho methali hufurahisha na kustarehesha, ndio maana, methali husimuliwa/huzungumzwa maranyingi jioni. Huu ni wakati baada ya saa nyinyingi za kazi nzito.

## **Huonya, hurudi na hushauri jamii**

Kwa kawaida watu katika jamii watoto kwa vijana huonywa na kuaswa kuwa na tabia njema na mwenendo mzuri na kufuata maadili mema ya jamii.

Mfano: “**Asiyesikia la mkuu huvunjika guu**”

## **Kuwakosoa na kukejeli**

Methali hukosoa na kukejeli wale wanaofanya kinyume na utaratibu wa jamii.

Mfano: “**Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno**”

## **Hutunza historia ya jamii**

Methali hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

## **➤ VITENDAWILI**

Kitendawili ni usemi uliofumbwa ambao hutolewa kwa hadhira ili ufumbuliwe. Fumbo hilo kwa kawaida huwa linafahamika katika jamii hiyo, na maranyingi lina mafunzo muhimu kwa washiriki mbali na kuwa chemsha zao.

Mfano: -Anatega huku akitambaa..... (BOGA)

-Akivaa nguo hapendezi, akiwa uchi yuapendeza mno.....(NDIZI)

-Amefunika kote kwa blanketi lake jeusi.....(GIZA)

- Amchukuapo hamrudishi.....(KABURI)

- Afahamu kuchora lakini hafahamu achoracho.....(KONOKONO)

- Anakula chakula cha afya bali hanoni.....(SUFURIA)

## **Fani katika vitendawili**

### **- Muundo**

Vitendawili huwa na muundo tofauti ukilinganisha na tanzu nyingine za fasihi simulizi. Muundo wa kitendawili unawenza kuwa ufuatao:

- Kitangulizi (mtambaji/mtegaji)

Mfano: Kitendawili....tega....(mteguaji)

- Kitendawili au swali/ fumbo lenyewe (mtegaji)

Mfano: “Ajenga ingawa hana mikono”

- Swali la msaada (mtegaji)

Mfano: Nini hicho?

- Kichocheo – Kichocheo hutolewa ikwa mteguaji ameshindwa kujibu.  
Kichocheo hutolewa na mtegaji.
- Jibu la fumbo (mteguaji)  
Mfano: NDEGE.

### - **Mtindo**

Vitendawili vina mtindo wa majibizano kati ya mtambaji na wasikilizaji. Mtambaji hutoa kitendawili, wasikilzaji hutakiwa kujibu.

### - **Matumizi ya lugha**

Vitendawili huwa vina utajiri mkubwa sana wa tamathali za semi na mbinu mbalimbali za kisanaa.

#### **Tamathali za semi**

##### **Sitiari**

Mfano: - Nyumba yangu haina mlango (yai)  
- Samaki wangu anaelea kimongomgongo (merikebu)

##### **Tabaini**

Mfano: -Yeye anatuona, sisi hatumwoni (Mungu)  
- Mkude ananiamkia, mdogo haniamkii (kunde kavu na mbichi)

##### **Kejeli/ Dhihaka**

Mfano: - Uzi mwembamba umefunga dume kubwa (usingizi)  
- Upara wa Mwarabu unafuka moshi (chai ya maziwa)

##### **Tashihisi**

Mfano: - Popo mbili zavuka mto (macho)  
- Popote niendapo ananifuata (kivuli)

#### **Mbinu nyingine za kisanaa**

##### **Onomatopea / Tanakali sauti**

Mfano: - Huku pi kule kule pi (mkia wa kondoo atembeapo)  
- Chubwi aingie chubwi katoka (jiwe majini)

##### **Takriri**

Mfano: - Huku fungu, huku fungu katikati bahari (nazi)  
- Mama kazaa mtoto na mtoto na mtoto kazaa mtoto (kuku na yai)

##### **Taswira/ Picha**

Mfano: - Kuku wangu katagia mibani (nanasi)  
- Mzazi ana miguu bali mzaliwa hana (kuku na yai)  
- Pana ng'ombe mionganoni mwa kundi la ndama (mwezi na nyota)

## **Maudhui na kazi ya vitendawili**

Je, vitendawili vina kazi gani?

- (a) **Kuelimisha:** Vitendawili huwa na upana mkubwa wa kimaudhui jambo ambalo huvifanya view nyenzo kubwa ya kuielimisha jamii hasa katika jamii au tamaduni simulizi, ambapo mfumo wa maandishi na usomaji haujashika sana.
- (b) **Kustarehesha na kupumbaza:** Hili ni jukumu linalojulikana tangu zamani, kuwa vitendawili huwa burudani kwa wanaohusika. Utegaji na uteguaji wa vitendawili hufanywa kwa njia inayowafanya wahusika kujipumbaza na kuitisha wakati kwa njia nzuri.
- (c) **Kusambaza elimu na ujuzi wa lugha:** Vitendawili huweza kutumiwa kama njia ya kuitisha mawazo muhimu kuhusiana na elimu ya jamii.  
Vitendawili kama kipengele cha fasihi smulizi kilikuwa nyenzo kuu ya kuielimisha jamii sio tu kwa kuijuza masuala muhimu bali pia kwa kuizoeza masuala yanayohusiana na lugha nyingine.
- (d) **Kudhihaki na kukejeli:** Vitendawili vina sifa ya kukejeli na kuwadhihaki watu fulani kwa kuyatumia majina yao kama msingi wa ulinganishi kwenye muundo wa kitendawili kinachohusika.  
Mfano: “ Mzungu katupwa jalalani”
- (e) **Hutumiwa kama chemsha bongo:** Hii ni njia nzuri ya kuujaribu uwezo wa msikilizaji wa kuyakumbuka masuala au mambo fulani, matukio muhimu na mambo yanayohusiana na historia na mazingira.
- (f) **Kupitisha maarifa:** Tumeona kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya vitendawili na methali. Basi tunaweza kusema kusema kuwa vitendawili ni njia nzuri ya kuitisha maarifa ya tanzu nyinginezo.
- (g) **Kuchochea udadisi:** Vitendawili hutumiwa kusaidia kujenga tabia ya udadisi na kutaka kufichua mambo.

### ➤ **NAHAU**

Nahau ni semi fupifupi ambazo hutumia maneno ya kawaida lakini maneno hayo hutoa maana tofauti na ile iliyokusudiwa.

Japokuwa nahau hutumia maneno ya kawaida lakini kauli yake ina undani kiasi kwamba kwa wageni wasiofahamu lugha hiyo hawawezi kuelewa maana.

Mfano: - Amina amevunja ungo.

- Sungura ameaga dunia.
- Lupinga amepata jiko.

### **Sifa za kutambulisha nahau**

#### **- Nahau kuwa sawa na neno kimaana:**

Nahau ikiwa ni fungu la maneno, wakati huo ni sawa na neon kimaana, yaani maana yake

Haijumuishwi kutokana na maana ya neon moja lililomo ndani ya fungu hilo. Jambo lenye kuthibitisha hayo ni kwamba nahau fulani zinaweza kufasiliwa kwa neno moja kwa kufichwa wazo halisi la nahau hii na myingine.

Mfano – Kupata jiko – kuoa

- Kushika hatamu - kuongoza
- Mtoto wa kikopo – mhuni
- Kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa – kudanganya.

### **- Nahau kuwa na maana ya kisarufi**

Nahau za Kiswahili huweza kulinganishwa na kitenzi, jina, kivumishi au kielezi. Nahau za Kiswahili tunaweza kuzigawanya katika makundi manne ya msingi.

#### **(i) Nahau - majina**

- Joka la mdimu
- Donda ndugu
- Ndege mbaya

#### **(ii) Nahau - vitenzi**

- Kufua dafu
- Kuvimba kichwa
- Kwenda joshi

#### **(iii) Nahau - vivumishi**

- a miraba minne
- a kufuta machozi
- a kijungujiko

#### **(iv) Nahau - vielezi**

- Bega kwa bega
- Kufa kupona
- Shingo upande

### **Mitindo ya Muundo wa Nahau**

Nahau za Kiswahili zinaweza kuundwa kwa mitindo mbalimbali. Mitindo iliyo maarufu zaidi ni kama ifuatayo:

- **T + N – Kukaanga mbuyu**
  - Kuwa macho
  - Kushikilia mkia
- **T+ N+E au V – Ana mkono mrefu**
  - Amefunga pingu za maisha
  - Amekula chumvi nyingi
- **T+T – Kufa kupona**
  - Patashika
- **T+E – Kujikaza kisabuni**
  - Kufa kikondoo
  - Kutokea puani
- **N+T – Akili kumruka**
  - Kiroho kinamdunda

Hii inaonesha kwamba nahau zote zimeundwa kwa mitindo sawa na ile ya mafungu ya maneno na hata sentensi zilizokuwa chanzo cha asili ya nahau zinazohusika.

## ➤ MISEMO

Misemo ni fungu la maneno linalototumiwa na jami ya watu kwa namna maalumu ili kutoa maana fulani.

### Au

Ni kauli yenyeye ukweli wa jumla inayotumiwa kusema mambo mbalimbali yanayouafiki ukweli huo.

Mfano: Mtu kwao

Maji hufuata mkondo

Misitu ni mali

Akili ni nywele

\*Maranyingi misemo huwa na upande mmoja ukilinganisha na methali ambazo huwa na pande mbili.

## ➤ MAFUMBO

Mafumbo ni kauli za maneno ya kawaida lakini zinazoficha maana. Kauli hizi hutumia lugha ya picha na tamathali.

Mafumbo huwa katika hali ya mazungumzo au vitendawili na huundwa kulingana na mazingira yanayohusika. Kwahiyoo, fumbo hilohilo litatumia maneno tofauti katika hali tofauti.

Mfano: - Hukaa katikati ya maadui lakini hawamuumizi (ULIMI)

- Kitendawili changu cha ajabu kina matone ya dhahabu (QURAN TUKUFU)

## ➤ LAKABU

Ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipatia kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia au kimatendo. Majina haya huwa ni maneno au mafungu ya maneno yenyeye maana iliyofumbwa. Baadhi ya majina humsifia mtu na mengine humkosoa au hata kumdhalilisha.

Mfano: Simba wa Yuda – Haile Selassie

Nyundo - Von Zelewiski

Mkuki uwakao - Jomo Kenyatta

Mti Mkavu - Jenerali Mayunga

## ➤ MIZUNGU

Ni kauli yenyeye picha za mafumbo na inaonesha ukinzani wa fikra au tukio. Mizungu hutumika kwenye soga na miviga. Kwa mfano, *Miti yote nitakwea mtarawanda unanishinda. Papai limeiva nyumbani, ila nashindwa kulila.*

Mizungu yote miwili inaeleza kuwa si vizuri kuoana ndugu wa damu. Mifano hiyo pia inaonesha kuwa jambo fulani linafaa au linawezekana lakini lingine halifai au haliwezekani. Ukinzani huu ni wa kawaida katika mizungu. Ukinzani huu unamfikirisha msikilizaji na kumpa changamoto ya kutafuta jibu.

## **(D) SANAA ZA MAONESHO**


Ni sanaa zilizo katika umbo lenye kutendeka. Sanaa za maonesho ni kitendo chochote chenye sifa kuu nne:

- Dhana ya kutendeka (Tendo)
- Mtendaji (Fanani)
- Uwanja wa kutenda (Mandhari)
- Watazamaji (Hadhira)

### **Vipera vya sanaa za maonesho.**

Sanaa za maonesho hujengwa kwa vipera vifuatavyo:

- Tambiko
- Miviga
- Majigambo
- Ngoma
- Michezo ya watoto
- Utani
- Ngonjera
- Vichekesho



## ➤ **TAMBIKO**

Ni ibada ya jadi inayoambatana na sadaka inayotolewa kwa Mwenyezi Mungu, miungu au mahoka, mizimu, pepo kwao binafsi au kupitia kwa Mwenyezi Mungu wakati wa kusalia miungu.

Matambiko yalikuwa na umuhimu mkubwa katika jamii za mababu zetu kuliko siku hizi. Jamii ya asili inapokabiliwa na matatizo yaliyowashinda kama vile magonjwa ya hatari, ukame na kukosa mtoto walifanya tambiko na kusali ili miungu iwasaide. Wakati mwingine jamii ilifanya tambiko kwa ajili ya kuomba radhi au kutoa heshima na shukrani.

### **Fani katika matambiko**

Katika tambiko sanaa inayotendeka ni ule ufundi wa kutenda vitendo kikamilifu.

Wahusika wa tambiko ni wale wazee maarufu walioteuliwa na jamii kuendesha shughuli hizi za matambiko.

Kwa upande wa mazingira, tambiko linaweza kufanyika porini au kwenye mti mkubwa au makaburini kutegemeana na tambiko lenyewe au jamii inayohusika.

### **Swali: Fafanua faida na hasara za tambiko katika jamii.**

#### **FAIDA:**

- Hujenga imani kama chombo cha kutatua matatizo katika jamii.
- Hujenga umoja na mshikamano.
- Hudumisha mila na desturi katika jamii

#### **HASARA:**

- Huwa na hasara ya kuua na kuharibu vitu.
- Hutumia gharama
- Huweza kuleta mfarakano wa jamii kati ya wanaoamini na wasioamini.

## ➤ **MIVIGA (SHEREHE)**

Miviga ni sherehe au shughuli zinazofanywa na jamii katika kipindi maalumu cha mwaka. Maranyingi kipindi hiki huwa ni baada ya mavuno ambapo watu huwa katika furaha ya kupata mavuno yao na kupumzika.

Miviga hufanywa na jamii kwa lengo la kufundisha jambo ama msingi fulani maalumu kwa maisha ya vijana waao. Sanaa za maonesho katika kundi hili linahusu kuingizwa kwa mwanajamii kwenye kundi la watu fulani kutoka kundi la watu wa aina nyingine. Kwa mfano; “Jando na unyago” kutoka katika kundi la watoto na kuingizwa kundi la watu wazima.

Miviga basi, huwa hasa ni ukabidhiwaji wa madaraka kwa anayehusika. Katika miviga kuna vipengele vingi lakini hapa tutazungumzia vipengele vikuu viwili ambavyo ni JANDO na UNYAGO.

Jando na unyago unahusu hatua tatu muhimu:

- (i) Kumtoa rasmi kijana kutoka katika kundi la watoto.
- (ii) Kumfundisha yote yahusikanayo na utu uzima kama vile:

- Umuhimu wa kazi
- Umuhimu wa ujasiri katika suala zima la ulinzi wa jamii nzima
- Suala la unymba na malezi bora kwa watoto.

- (iii) Kumwingiza rasmi katika kundi la watu wazima.

Kwa baadhi ya makabila, hatua ya kwanza hutekelezwa kwa kuwatahiri vijana wanaohusika. Hatua ya pili hutekelezwa kwa ngoma ambayo nyimbo na vitendo vyake ndivyo vinavyobeba mafunzo yote yanayohusu maisha ya vijana. Katika hatua hii watu wanaohusika katika kuwfundisha vijana huwa ni watu wazima ambaao huitwa “**MAKUNGWI**” kwa wasichana na “**NGARIBA**” kwa wavulana.

### **Fani za miviga (Jando na Unyago)**

Kwa upande wa wahusika katika jando na unyago, kuna watendaji na watazamaji. Wale wote wanaoshiriki ndiyo watendaji, wanaotenda ile dhana ya kuwatia vijana katika kundi la watu wazima.

Kwa upande wa watazamaji, ni wale vijana ambaao mambo ya jando na unyago yanafanyika kwa sababu yao.

Uwanja wa kutendea, ni mahali sherehe zinapochezwa. Inaweza ikawa ndani ya nyumba au porini, mlimani au mapangoni.

### **Swali: Fafanua umuhimu na hasara za miviga (Jando na unyago)**

#### ➤ **UTANI**

Ni hali ya kufanyiana mizaha au masihara baina ya watu pasipo kuogopana au kushitakiana tofauti na desturi ya kutoheshimiana.

Utani huweza kuwa kati ya mtu na mtu, ukoo na ukoo, kabila na kabila na kadhalika. Kwa kawaida watu wanaotaniana huwa wanaheshimiana na kusaidiana kama ndugu.

#### **Fani katika utani**

Kwa upande wa wahusika, wahusika wake huwa ni binadamu ambaao wanataniana.

Mazingira, mazingira ya utani huweza kuwa msibani, harusini au mahali popote.

### **Swali: Fafanua faida na hasara za utani katika jamii**

## ➤ NGOMA

Neno ngoma lina maana kadhaa.

- Ngoma ni chombo cha muziki.
- Ngoma pia ni uchezeshaji wa viungo vya mwili wenye mitindo na miondoko maalumu pengine ukiambatana na muziki.
- Ngoma pia ni sherehe iwe ni jando, arusi, unyago na kadhalika.

Ngoma inayoongelewa katika mada hii ni ile yenye maana ya pili – uchezeshaji wa viungo vya mwili wenye mitindo na miondoko maalum, pengine ukiambatana na muziki. Pia hapa zinaongelewa ngoma ambazo haziambatani na sherehe maalum, ngoma zile ambazo huchezwa zikiwa hazikufungwa kwenye mfumo wa sherehe yoyote na ngoma hizi huchezwa wakati wowote.

Mfano wa ngoma ni kama vile: Gombe Sugu(Wazaramo) Kitoto(Wangoni) Msunyunho (Wagogo) na kadhalika.

### **Fani katika ngoma**

Sanaa katika ngoma hubainishwa na ule ufundi wa uchezaji, yaani jinsi wale wachezaji wanavyocheza kwa kufuata milio ya ngoma na sauti za wimbo unaoimbwa katika ngoma hiyo.

Kwa upande wa wahusika, kuna wahusika wa aina mbili, watendaji (wachezaji) na watazamaji. Wachezaji ni wale wanaofanya tendo la kucheza na kuimba na watazamaji ni wale wanaotazama vitendo vinavyotendeka.

Uwanja wa kutenda ni sehemu yoyote yenye eneo la kutosha kuweza kucheza aina fulani ya ngoma. Inaweza kuwa uwajani au nje ya jumba lenye eneo kubwa la kuwezesha ngoma ya aina fulani ichezwe.

### **Swali: Fafanua faida na hasara za ngoma**

## ➤ MICHEZO YA WATOTO

Ni michezo mbalimbali inayochezwa na watoto. Michezo ya watoto wadogo hufungamana na hali halisi ya utamaduni, uchumi na siasa ya jamii inayohusika. Kwa kuwa fasihi simulizi ina dhima ya kutoa maadili kwa jamii, michezo ya watoto husaidia watoto waweze kujifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, utamaduni na siasa ya jamii yao.

Watoto katika michezo yao huiga mambo halisi yanayofanyika katika jamii yao. Mambo hayo ni kama vile: Kulima, kulea watoto, kutwanga, kupika na kadhalika.

Kuna michezo mingi ya watoto kama vile kuigiza baba na mama, kutengeneza vifaa, kuruka kamba inayozungushwa, kujificha, kuimba nyimbo na kadhalika.

### **Fani katika michezo ya watoto**

Kwa upande wa wahusika ni watoto wenyewe wanaocheza michezo hiyo, yaani wavulana na wasichana. Idadi ya wahusika inategemea michezo wenyewe wanaocheza.

Uwanja wa kutenda michezo ya watoto ni sehemu yoyote itakayochaguliwa na watoto wenyewe kulingana na mchezo wenyewe. Kwa mfano wanaweza kucheza uwanjani, chini ya mti, barabarani, kando ya nyumba, ndani ya nyumba na kadhalika.

Kwa upande wa lugha, michezo ya watoto wadogo inatumia lugha ya jamii inayohusika, yaani lugha mama. Lakini sehemu za mjini ambamo Kiswahili hutumika sana, lugha inayotumiwa na watoto katika michezo yao ni Kiswahili.

**Swali: Fafanua umuhimu na hasara za michezo ya watoto**

➤ **VICHEKESHO**

Ni mpangilio wa maneno ambayo yanawasilisha ujumbe fulani maalum kwa njia ya kuchekesha au kufurahisha. Kimuundo, vichekesho huwa ni vifupi na havihitaji uchambuzi mpevu au wa ndani ili kupata maana nyingine ya ndani.

Lugha yake huweza kuwa nyepesi na iliyojaa picha ambazo watazamaji wana uwezo wa kuzitambua.


➤ **MICHEZO YA JUKWAANI**

Ni mpangilio wa mazungumzo baina ya watu unaoambatana na utendaji. Mazungumzo hayo yanajenga kisa chenye mgogoro fulani wa kijamii.

Michezo inayoigizwa jukwaani ni ya kila aina. Kuna michezo ya kawaida inayoambatana na sauti na mingine isiyoambatana na sauti (Onesho bubu). Kimsingi vitanzu hivi huhusisha utendaji ambao unategemea matumizi ya ishara za mikono na sehemu nyingine za mwili pasipokuwa na maana.

**TANBIHI:** Majigambo na Ngonjera vipera hivyo vimejadiliwa katika utanzu wa ushairi.

## **Mchoro wa fasihi simulizi wenye tanzu na vipera vyake**



### **Vipengele muhimu vya fasihi simulizi**

#### **(a) Msimulizi (fanani)**

Huyu huwa ni mtu ambaye anaitamba hadithi, kuimba wimbo, kutoa kitendawili, metha na kadhalika

#### **(b) Wasikilizaji au watazamaji (hadhira)**

Hawa huwa ni washiriki katika kutazama au kusikiliza fani za fasihi simulizi na maranyingine huwa wanatumiwa na fanani kama wahusika wa fani yake.

#### **(c) Pahali /Mazingira**

Hapa huwa ni jukwaa au pahali ambapo tukio la fasihi simulizi linatendeka. Pahali hapo panaweza kuwa nyumbani, uwanjani, kuzunguka moto, baharini na kadhalika.

#### **(d) Tukio**

Hili huwa ni tendo linalotendeka katika jukwaa la fasihi simulizi. Tendo hilo linaweza kuwa ni usimuliasi wa hadithi, kutega vitendawili, kuimba nyimbo au kutoa methali.

### **UHIFADHI WA FASIHI SIMULIZI**

Kazi za fasihi simulizi zimeanza tangu binadamu walipoanza kupambana na mazingira yao ya kuishi pamoja. Kazi hizo zilisimuliwa na kuakisi shughuli mbalimbali zilizokuwa zikifanywa na watu katika mazingira ya wakati huo. Kadiri mazingira yalivyobadilika na mambo yaliyosimuliwa yalibadilika. Hivyo kulikuwepo na haja ya kuhifadhi kazi hizo. Katika kuhifadhi kazi hizo, kuna njia mbalimbali zilizotumika.

### **Nja za kuhifadhi fasihi simulizi**

Kuna njia mbalimbali zinazotumika katika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. Njia hizo ni:

**(a) Kichwani /Akilini**

Hii ni njia mojawapo inayotumika katika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. Njia hii maranyingi hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hii ni njia kongwe mno, kwani ilianza kabla hata ya vyombo ambavyo ni matokeo ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Fasihi simulizi ikihifadhiwa kichwani huendelea kuwa hai kwani hadhira na fanani huwasiliana ana kwa ana. Hadhira inaweza kumpongeza au kumhoji fanani papo kwa papo.

**Udhaifu wa fasihi simulizi ikihifadhiwa kichwani**

- Kusahau kwa fanani
- Kufa kwa fanani au msimuliaji.
- Msimuliaji anaweza kuacha mambo muhimu.

**Faida za kuhifadhi kichwani**

- Baadhi ya mambo huweza kupatikana kwa uhalisia. Mfano, vitendo
- Huweza kuenezwa kwa watu wengi. Yaani wote wanaojua na hata wasiojua kusoma na kuandika.

**(b) Maandishi**

Fasihi simulizi huweza kuhifadhiwa katika maandishi. Mfano kwenye vitabu, vijarida na kadhalika. Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika njia hii, haibadiliki na kuwa fasihi andishi bali itabaki fasihi simulizi ileile. Kinachofanyika hapa ni kuchukua vipera vya fasihi simulizi na kuviveka katika maandishi ili kuipendezesha kazi hiyo.

**Udhaifu wa njia hii**

- Hutumika gharama katika kuhifadhi kazi hiyo.
- Inabagua, kwani inahusisha wale tu wanaojua kusoma na kuandika.
- Haipokei mabadiliko ya papo kwa papo.
- Baadhi ya vitendo havioneekani.

**Faida za njia hii**

- Hutunza kumbukumbu kwa muda mrefu

**(c) Vinasa sauti**

Hizi ni zana zitumikazo kurekodi sauti. Zana hizo ni kama vile tepurekoda, santuri na kadhalika.

Katika njia hii ukweli wa sanaa ya kazi haitabadilika. Vifaa hivi ni matokeo ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

**Udhaifu wa njia hii**

- Gharama
- Kutobadilika kulingana na mazingira na wakati.
- Utendaji wa wahusika hauoneekani
- Zana hizo zinaweza kuharibika au kupotea.

### **Faida za njia hii**

- Sauti za watusika zitasikika
- Inatunza kumbukumbu kwa muda mrefu.

#### **(d) Kanda za video, runinga, tarakilishi na filamu za sinema**

Kanda za video hurekodi sauti na sura. Picha hizo huoneshwa kwenye video au runinga. Picha za sinema hupigwa kwa aina maalumu za kamera ambazo huoneshwa kwa projekta na kuonekana zinatembea.

### **Udhaifu wa njia hii**

- Gharama
- Haipokei mabadiliko kulingana na mazingira na wakati
- Zana hizo zinaweza kuharibika au kupotea
- Fanani hawezi kuonana na hadhira yake.

### **Faida za njia hii**

- Huweza kudumu kwa muda mrefu.
- Matendo na sauti za watusika husikika

#### **TANBIHI:**

Faida na hasara za njia hii zipo nyingi, kila mmoja anaweza kuzitaja kulingana na mtazamo wake pia, ingawa mtazamo usiathiri uhalisia wa jambo.

### **Umuhimu wa kuhifadhi kazi za fasihi simulizi**

Kuna faida mbalimbali za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. Miongoni mwa faida hizo ni:

- (i) **Kutopotea kwa kazi hizo;** ikiwa msimulaji wa kazi hizo atahifadhi kazi hizo  
uwezekano wa kupotea ni mdogo. Ndiyo maana mpaka leo  
hii tunazikiliza kazi za zamani kwa zimehifadhiwa.

- (ii) **Kutunza amali za jamii;** kwa kuhifadhi nyimbo na kazi zingine za kisanaa ni tuzo  
na kumbukumbu tosha kwa vizazi vujavyo. Sanaa ni amali  
ya jamii.

### **Ukusanyaji wa fasihi simulizi**

Ili kuhifadhi kazi za fasihi simulizi ni lazima kwanza zikusanywe. Kazi hizi zinaweza  
kukusanywa kwa:

- (i) **Wakisikiliza wasanii wakisimulia na kuzitamba kazi zao.** Hivyo fanani anaweza  
kusikiliza, akaziandika au akazirekodi tayari kwa kuzihifadhi kwenye kichwa, vinasa  
sauti, filamu au maandishi.

- (ii) **Kujiunga na wacheza bao ambao pia wanapiga soga na kusimulia hadithi  
mbalimbali.**

Mkusanyaji anasikiliza kwa makini na kuzihifadhi kichwani au akilini. Baada ya  
masimulizi hayo anaweza kuziandika ili kuzihifadhi kwa njia bora nay a kudumu  
zaidi.

- (iii) **Kuwatembelea wazee ambao ni mashuhuri katika kutamba hadithi, kughani  
mashairi au kutumia misemo na methali.**

### **Kukua na kuenea kwa fasihi simulizi**

Kwa hivi sasa hapa nchini, kuna mambo mbalimbali yanayosaidia katika kukua na kuenea

kwa fasihi simulizi. Mamba hayo ni:

**Mfumo wa elimu, mfumo wa elimu unasaidia katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.**

Kwa sasa Fasihi simulizi ni somo linalofundishwa toka darasa la kwanza hadi chuo kikuu. Sanaa za maonesho hufundishwa katika vyuo kama vile (Bagamoyo, Butimba)

Mengistu Machaku